# Nipashe

Jumamosi Septemba 17, 2022 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • Na. 0581071


www.ippmedia.com

www.twitter.com/nipashetz www.facebook.com/nipashetz www.instagram.com/theguardian_newspaper LIKE & FOLLOW US




SUPA JACKPOT TZS. 1,031,243,893 KWA TZS. 1000 TU!

SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU! SportPesa.CO.TZ PIGA *150*87#

**Balozi** Rupia afariki dunia, Samia amlilia

UKURASA 3



HARMONIZE, KAJALA HAYUPO WA KUWASUMBUA

UKURASA 12

SAKATA PANYA ROAD

# Masauni, Wambura wakunjua makucha

UKURASA 2







Baadhi ya magari yaliyowahi kukumbana na kamata kamata inayofanywa na wafanyakazi wa Wakala wa Mabasi Yaendayo Haraka Dar es Salaam (DART), yakitumia barabara za mabasi hayo kinyume cha sheria. **PICHA ZOTE: MTANDAO**

## TUCTA yatoa kauli kikokotoo cha asilimia 33

UKURASA 3

## Polisi yaonya matumizi holela ya barabara za mwendokasi

UKURASA 2



**MICHEZO** YANGA YAKAMILISHA MAWINDO YA ZALAN UK.24

**KABWELA** UK.18



Rais wa Zanzibar, Alhaj Dk. Hussein Ali Mwinyi akisalimiana na Mufti Mkuu wa Zanzibar, Shekhe Saleh Omar Kabi, baada ya kumalizika kwa Swala ya Ijumaa, katika Masjid Jamiu Zinjibar Mazizini Wilaya ya Magharibi "B" Unguja jana. Kushoto ni Balozi Mdogo wa Oman anayefanyia kazi zake Zanzibar, Said Salim Al-sinawi. **PICHA: IKULU**

# Masauni, IGP wakunjua makucha 'Panya Road'

**Na Waandishi Wetu**

WAKATI Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Hamad Yusuph Masauni, akionya wanaounga mkono vijana wa 'Panya Road', Mkuu wa Jeshi la Polisi nchini, Inspekta Jenerali (IGP) Camilius Wambura, ameitahadharisha kundi hilo kukaa chonjo kwa kuwa huu ni wakati mbaya kwao.

Wakizungumza jana jijini Dodoma kuhusiana na hali ya usalama nchini na hatua zilizochukuliwa kudhibiti vikundi hivyo, walisema wanunuzi wa bidhaa au mali za wizi zinazotokana na uporaji unaofanywa na "Panya Road" nao hawako salama.

"Kama kuna mtu ambaye ananunua bidhaa hizi au mali za wizi na yeye ajue kwamba hayuko salama. Na kama kuna mzazi anashiriki kwa namna yoyote ile kwenye uhalifu huu, kwa kutumia mali za wizi au kushiriki kwa namna yeyote ile, hayuko salama.

"Naomba nitoe tahadhari sana kwa jamii, watambue kwamba tuko 'very serious' (umakini sana) na uhai wa watu au usalama wa raia wa nchi hii. Sielezi mikakati gani imefanyika, lakini kuna mambo mazito ambayo hata IGP mwenyewe hataweza kuyazungumza hadharani.

Baada ya kauli ya Waziri Masauni, IGP Camillius Wambura alieleza jeshi hilo lilivyojiandaa kuwakabili 'Panya Road'.

"Sasa hawa (Panya Road), napenda nichukue nafasi hii kuwaonya. Ninawaonya sana na ninawaonya vikali. Mambo waliyokwisha kuyafanya, hayakubaliki na hatutakaa tukubali jambo hili.

"Kama hawaoni kinachoendelea naamini wanao ndugu zao ambao wana nafasi ya kusoma magazeti, kuangalia televisheni na kusikiliza redio wawafikishie ujumbe, wakae chonjo.

"Huu ni wakati mbaya kwao. Ninachojaribu kukifikiria sijui kama hawa wahalifu wanajua wanapambana na nani? Mimi ninachojua uhalifu huu wa kwenda kupeleka madhara kwa wananchi wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, wanapambana na serikali," alisema.

IGP Wambura alisisitiza kuwa serikali kupitia Jeshi la Polisi, haijawahi kushindwa dhidi ya mhalifu yeyote na hakuna mhalifu ambaye ameshindana na serikali akashinda.

"Ujumbe huu uwafikie popote walipo, wote wanaosikiliza kwa niaba yao wawafikishie habari wakae chonjo, saa ni mbaya dhidi yao," alisema.

DC MWEGELO AAPA

Mkuu wa Wilaya ya Temeke, Jokate Mwegelo, ambaye wilayani kwake vikundi hivyo vilivamia kata tatu za Mianzini, Chamazi na Kilungule Septemba 12 na 13, mwaka huu, ameapa kuwa atapambana nao na kuwaonya wanaojihusisha na vitendo hivyo kuwa hawataachwa salama.

Mwegelo alisema wameshaanza kuchukua hatua dhidi ya wahalifu hao na kwamba mpaka jana, zaidi ya watuhumiwa wa uhalifu 100, wakiwamo wa vijana wa 'Panya Road' wamekamatwa.

"Sitakubali katika uongozi wangu Temeke iingie kwenye dosari ya vitendo vya uhalifu ndiyo maana katika hili tutakula sahani moja. Hatuwezi kuwa tunapangiwa kazi na vijana wa ovyo," alionya.

Usiku wa kuamkia Jumanne huko Mbagala Maji Matitu, zaidi ya vijana 20 walivamia nyumba mbili maeneo hayo na kujeruhi kisha kuiba televisheni mbili na siku iliyofuata walionekana Chamazi ambako walidhibitiwa.

Siku nne zilizopoita, Jeshi la Polisi Kanda Maalum ya Dar es Salaam, lilitangaza kuwashikilia watuhuniwa 116 wanaodaiwa kujihusisha na vitendo vya uvunjaji wa nyumba na kupora mali, wakiwa na silaha mbalimbali za jadi.

Aidha, siku tatu zilizopita, vijana hao walivamia maeneo ya Kawe Mzimuni ambako walijeruhi na kusababisha kifo cha mwanafunzi wa mwaka wa pili wa Shule Kuu ya Uandishi wa Habari Dar es Salaam (SJMC) ambako pia walipora mali mbalimbali.

Kikundi cha Panya Road kiliibuka Aprili, mwaka huu, na kufanya matukio katika maeneo mbalimbali ya Dar es Salaam yakiwamo Chanika, Kitunda, Tabata, Mbezi, Kinyerezi na Kunduchi.

Kutokana na kukithiri kwa vitendo hiyo, juzi, wabunge waliitaka serikali ichukue hatua madhubuti kuyadhibiti kwa kuwa yanatishia maisha na usalama wa raia na mali zao.

Spika wa Bunge, Dk. Tulia Ackson aliiagiza serikali kushughulikia jambo hilo kwa haraka.

■ **Imeandaliwa na Godfrey Mushi (Dodoma) na Romana Mallya (DAR).**

# Polisi yaonya matumizi holela ya barabara za mwendokasi

**Na Romana Mallya**

VIDEO fupi ikionyesha mzozo kati ya wafanyakazi wa Wakala wa Mabasi Yaendayo Haraka (BRT) na askari polisi waliopita barabara ya mwendokasi, imeliibua Jeshi la Polisi nchini na kuonya kuwa hakuna mwenye mamlaka kupita eneo hilo hata kama ni watu wenye nyadhifa na vyeo isipokuwa wenye dharura maalum pekee.

Akizungumza na Nipashe jana, Msemaji wa Jeshi la Polisi nchini, Kamishna msaidizi Mwandamizi (SACP) David Misime, alisema kwa mujibu wa Sheria ya Usalama Barabarani kifungu namba 54, magari ambayo yanaweza kupita popote lakini yakiwa yanakwenda katika dharura.

"Mfano, polisi amepewa taarifa ya tukio la ujambazi au watu wanavamia mahali, wanaweza kutumia barabara yoyote kama kuna udharura, zimamoto wanawahi tukio la moto, gari la wagonjwa ndiyo dharura na sheria imeeleza hivyo.

"Siyo mtu anakwenda kazini au wapi anaamua kupita mwendokasi. Ni dharura pekee ndiyo sheria inaruhusu. Wengine wanatafsiri magari ya dharura kwa sababu limeandikwa namba ya jeshi basi litapita tu. Lina dharura gani? Ulikuwa unakimbilia tukio gani? Ulikuwa unawahi kuchukua mgonjwa? Ulikuwa unawahi kwenye tukio la moto," alihoji.

Taarifa iliyotolewa juzi na Misime baada ya kusambaa kwa video hiyo, ilisema si kwa raia wala kwa mtu mwenye cheo cha aina yoyote, awe anaendesha au kuendeshwa, haruhusiwi kupita katika barabara hiyo isipokuwa mabasi ya mradi huo.

Misime alisema Jeshi la Polisi linatoa onyo hilo kuwa hakuna chombo chochote cha moto, baiskeli, mkokoteni au guta kinachoruhusiwa kupita barabara ya mwendokasi zaidi ya mabasi yenyewe.

"Yeyote atakayepita au kulazimisha kupita katika barabara za mwendo kasi atachukuliwa hatua za kisheria ikiwa ni pamoja na kujulisha mamlaka anayotoka kama ni mtumishi wa umma, ili hatua za kinidhamu ziweze kuchukuliwa dhidi yake," alisema.

Mara kwa mara baadhi ya magari ya taasisi, mashirika, kampuni na watu binafsi wakati kukiwa na foleni kwenye barabara za kawaida, yamekuwa yakipita kwenye barabara za mwendokasi na kuna ajali zimewahi kutokea kutokana na kitendo hicho.

HABARI KITAIFA

# TUCTA yafurahia kikokotoo kipya mafao cha asilimia 33

**Na Renatha Msungu, DODOMA**

SHIRIKISHO la Vyama vya Wafanyakazi Tanzania (TUCTA), limesema kikokotoo kipya cha mafao ya wastaafu cha asilimia 33 kimelenga kumkomboa mtumishi wa umma.

Akizungumza na waandishi wa habari jana jijini hapa baada ya kuhitimisha kikao cha Baraza Kuu la TUCTA, Mjumbe wa baraza hilo, Emmanuel Mwakajila, alimpongeza Rais Samia Suluhu Hassan kwa kuonyesha dhamira hiyo ya dhati.

Pia baraza hilo limempongeza Rais Samia kwa kuwapa mafunzo kuhusu kikokotoo hicho kipya kuwajengea uelewa ili kufikisha elimu hiyo kwa wafanyakazi. Mwakajila alisema wameona sheria hiyo ni nzuri na wataelimisha wafanyakazi waielewe.

"Mtakumbuka Mei Mosi, mwaka huu, Rais Samia aliwatangazia wafanyakazi kwamba amekubali ombi la wafanyakazi kufikia kikokotoo cha asilimia 33 wanapostaafu na kuachana na kile cha zamani cha asilimia 25," alisema.

Pamoja na mabadiliko hayo, Mwakajila alisema kumeibuka upotoshaji ambao umezagaa kwamba kikokotoo hicho kitanyonya haki za wafanyakazi wa sekta binafsi na watumishi wa umma.

"Mafunzo haya yaliyotolewa yameonyesha dhamira njema ya serikali iliyopo madarakani ya kuhakikisha mtumishi anapostaafu kila mwisho wa mwezi atakuwa anapokea kiasi kikubwa cha pensheni, tofauti na kikotoo cha asilimia 25.

"Hii inaweka uhakika wa maisha ya mfanyakazi baada ya kustaafu. Kwa muda mrefu vikokotoo hivi vilikuwa havitendi haki kwa maana, kikokotoo cha zamani cha asilimia 25 kilikuwa kinawapa faida watu wachache ambao walikuwa wakipata asilimia 50," alisema.

Alisema kwa sheria na kanuni hiyo mpya, wafanyakazi na watumishi wa sekta zote watafurahia mafao ya usawa, likiwa ni takwa la kikatiba la kuhakikisha sheria za nchi zinazotungwa zinakuwa zile zinazozingatia usawa.

"Kwa kikokotoo cha asilimia 25, kwa mtaalam yeyote ataona ulikuwa ubaguzi katika suala zima la ajira na wote wanachangia sawa lakini mmoja analipwa kwa asilimia 25 na mwingine analipwa kwa asilimia 50," alisema.

Mwakajila alisema kanuni hiyo mpya ya kikokotoo itaweka uhimilivu wa mifuko wa hifadhi ya jamii na kuuletea afya na uhakika kwa watumishi kunufaika na mafao.

Pia alisema kanuni hiyo mpya ya mafao, itaruhusu mtumishi kabla hajastaafu, kupata mikopo ya ziada ili aanze kuandaa makazi yake na baada ya kustaafu, atakuwa anapata pensheni ya mwezi sawa na mshahara wake wa mwisho aliokuwa anaupata.

"Tunaona kuna uhakika mkubwa, Rais Samia ameingia madarakani na kukuta mifuko hiyo ikiwa na madeni makubwa lakini amelipa zaidi ya Sh. bilioni 700 ili kunusuru hali ya mifuko," alisema.

## Wafanyabiashara kulipa malimbikizo kwa awamu

**Na Rahma Taratibu (SJMC)**

Serikali kupitia Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) inaendelea kujadiliana na wafanyabiashara wenye malimbikizo ya kodi ili kuwapa unafuu wa kulipa kwa awamu bila kuathiri ukwasi, mwenendo na uendeshaji wa biashara.

Naibu Waziri wa Fedha na Mipango, Hamad Hassan Chande, alisema hayo jana Bungeni jijini Dodoma wakati akijibu swali la Mbunge wa Viti Maalum, Asha Abdullah Juma, kuhusu hatua zinazochukuliwa kwa walipakodi walioshindwa kulipa na kuwa na malimbikizo makubwa lakini wako tayari kulipa kutokana na agizo la Rais.

"Sheria ya Usimamizi wa Mapato, Sura 438 Kifungu cha 70 na Kanuni zake, kinampa mamlaka Kamishna Mkuu wa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) kusamehe adhabu na riba kama kuna suala na sababu maalum," alisema.

Katika hatua nyingine, Chande alisema serikali ilifuta utaratibu kwa walipakodi kulipa kodi kabla ya kuanza biashara ili kutoa nafasi ya kujiimarisha kibiashara.

Alisema hayo alipojibu swali la Mbunge wa Viti Maalum, Zainab Katimba, aliyetaka kujua muda ambao serikali itaondoa utaratibu wa biashara mpya kutakiwa kulipa kodi ya mapato kabla ya kuanza.

Chande alisema, mwaka 2019/20 serikali ilifuta utaratibu wa walipakodi wote wanatakiwa kulipa kodi miezi sita baada ya kufungua biashara na kuongeza kuwa utozaji wa kodi ya mapato hufanyika kulingana na mapato yaliyopatikana katika kipindi cha mwaka husika.

Aidha, aliiagiza TRA kuendelea kufuata sheria, utaratibu na kanuni zilizowekwa na serikali katika kutekeleza majukumu ya kila siku.



Mafundi wa Kampuni ya Sino, wakiendelea na ujenzi wa kituo cha mabasi yaendayo haraka (BRT), katika Barabara ya Kilwa, Mtoni Mtongani mkoani Dar es Salaam jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Balozi Rupia afariki dunia, Samia amlilia

**Na Romana Mallya**

KATIBU Mkuu Kiongozi mstaafu, Balozi Paul Rupia (84), amefariki dunia asubuhi nchini Afrika Kusini, alikokuwa akiendelea na matibabu ya maradhi yaliyokuwa yakimkabili.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa na mtoto wa marehemu, Peter Rupia, Balozi Rupia alifariki jana asubuhi.

Kutokana na kifo hicho, Rais Samia Suluhu Hassan katika ukurasa wake wa Twitter, aliandika jana: "Nimepokea kwa masikitiko taarifa za kifo cha Katibu Mkuu Kiongozi Mstaafu, Balozi Paul Rupia,

"Tumeondokewa na mtu aliyetoa mchango mkubwa katika masuala ya kidiplomasia, mageuzi ya kiuchumi na utumishi wa umma na aliyeweka mbele maslahi ya taifa. Mungu amweke mahali pema. Amina."

Msemaji Mkuu wa Serikali, Gerson Msigwa, alisema Balozi Rupia alikuwa Katibu Mkuu Kiongozi kati ya mwaka 1986 na 1994, akichukua nafasi ya Timoth Apiyo.

"Alitoa mchango mkubwa sana alikuwa mwanadiplomasia mzuri. alikuwa Katibu Mkuu Kiongozi katika kipindi ambacho nchi ilifanya mageuzi makubwa ya kiuchumi kuanzia awamu ya pili utawala wa Rais Ali Hassan Mwinyi. Wakati huo kulikuwa na mageuzi ya uchumi huru, soko huru.

"Na Katibu Mkuu Kiongozi ndiye mshauri wa karibu wa Rais, wakati ule kulifanyika mabadiliko makubwa kwenye utumishi wa umma. Alikuwa mtu mwema aliishi vizuri na viongozi na watumishi, na alikuwa mbunifu wa namna bora kuboresha uchumi," alisema.

Msigwa alisema alikuwa mtu mahiri kwenye diplomasia, alijua kuitangaza nchi kimataifa, alikuwa mwadilifu, mzalendo.

Aliwahi kuwa ofisa katika Wizara ya Mambo ya Nje kuanzia mwaka 1963 na Balozi wa Tanzania katika nchi mbalimbali ikiwamo Uingereza na baadaye Balozi wa Tanzania katika Umoja wa Mataifa.

Pia aliwahi kuwa Katibu Mkuu Wizara ya Mambo ya Nchi za Nje na Ushirikiano wa Kimataifa na Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi ya Benki ya Watu wa Dar es Salaam.

Balozi Rupia ni mtoto wa mpigania uhuru, mwanasiasa na mfanyabiashara wa zamani, John Rupia, ambaye alikuwa mwasisi wa Chama cha Tanganyika African Association (TAA), Tanganyika African National Union (TANU) na African Association (AA).

**MAKATIBU WAKUU KIONGOZI**

Makatibu Wakuu Kiongozi waliopita ni pamoja na Dunstan Omary (1962- 1964), Joseph Namata (1964-1967), Dickson Nkembo (1967-1974),Timothy Apiyo (1974-1986), Paul Rupia (1986-1994) na Balozi Dk. Matern Lumbanga (1994-2006).

Wengine ni Philimon Luhanjo (2006-2011), Balozi Ombeni Sefue (2012-2016), Balozi John Kijazi (2016-2021), Balozi Dk. Bashiru Ally (2021) na Balozi Hussein Kattanga mwaka 2021 mpaka sasa.

# Godoro, pazia vyapokewa kortini kielelezo ushahidi kesi ya mauaji

**Na Grace Gurisha**

MAHAKAMA ya Hakimu Mkazi Kisutu, imepokea kielelezo cha godoro, pazia na nyavu ambavyo vinadaiwa kumfungia marehemu Farahani Maluni, na kumfukia mbele ya nyumba iliyoko Ilala Sharif Shamba, Dar es Salaam.

Uamuzi wa kupokea vielelelzo hivyo ulifikiwa jana mbele ya Hakimu Mkazi Mkuu Joyce Minde, baada ya aliyekuwa Mkuu wa Upelelezi wa Makosa ya Jinai, Mrakibu Msaidizi wa Polisi ASPO Leonard Makona, kuiomba mahakama ipokee vitu hivyo kama kielelezo kwenye kesi ya mauaji inayomkabili Hemed Ally.

ASP Makona, alidai vitu hivyo walivipata baada ya kuchimba kwenye nyumba ambayo alikuwa amepanga Ally na kukuta mabaki ya mifupa, fuvu na nyama nyama ambazo zilikuwa zimeoza.

Alidai walichukua muda mrefu sana kufukua, wakaanza kufikiria kuleta kifaa ili kiwasaidie, lakini ghafla wakaanza kuhisi harufu kali. Alidai kuwa wakati huo mshtakiwa Ally alikuwa anamwita pembeni na kumweleza wasogee mbele kidogo.

"Tukaanza kuona panzia, godoro dogo lililokuwa na 'cover' lake. Baada ya hapo tukaona mabaki ya mifupa ya miguu na mikono, fuvu na nyama zilizoharibika," alidai ASP Makona.

Baada ya kuona hayo, alidai walikwenda Mahakama ya Wilaya ya Ilala kuomba amri ya kuutoa mwili juu na walipewa amri hiyo na kufanya hivyo, ambapo waliona godoro na 'cover' lake, panzia, nyavu na fulana ambayo anahisi ilikuwa ya kazi.

ASP Makona, alidai walichukua mabaki hayo na kuyapeleka katika Hospitali ya Taifa Muhimbili kama amri ya mahakama ilivyoelezwa. Alidai kuwa Februari 10, mwaka huu, walikwenda hospitalini hapo wakiwa na ndugu wa marehemu, mke wa Maluni na watoto wakachukuliwa sampuli kwa ajili ya kupima vinasaba (DNA).

Pia, alidai walipata taarifa kuwa wakati Ally anatuhumiwa kufanya tukio hilo, aliihamishia familia yake kwa mama mkwe wake, Mtaa wa Faru, Kariakoo jijini Dar es Salaam. Alidai alimwagiza Koplo Apolonia, kwenda kufanya upekuzi na walikuta mapanzia 23 ambayo yanafanana na lile lililokutwa na mabaki ya marehemu.

Awali, ASP Makona alidai Februari 9, 2015 majira ya asubuhi akiwa ofisini kwake alipewa taarifa kwamba Ally anataka kumwona ambapo aliagiza apelekwe kwake, kabla ya mshitakiwa kuanza kuzungumza chochote akaanza kulia.

"Kweli nilimuua Maluli kwa sababu alikuwa ananisumbua sana. Ananidai Sh. milioni 30. Nilimwita nyumbani Ilala nilipokuwa naishi nikamnyonga kwa kutumia panzia na kisha kumfukia kwenye shimo nililochimba," alidai Mahona akinukuu kauli ya mshtakiwa.

Inadaiwa Juni 12, 2014 mshitakiwa Hemed Ally eneo la Sharif Shamba ndani ya Wilaya ya Ilala, Dar es Salaam, alimuua Farahani Maluni.

# Vijana wasomi wajiajiri biashara matunda

**Na Vitus Audax,** MWANZA

BAADHI ya wahitimu wa vyuo vikuu mbalimbali mkoani Mwanza wamejiajiri katika biashara za kuuza magenge ya bidhaa ndogo ndogo na matunda ili kujipatia kipato kutokana na kukosa ajira za kuajiriwa.

Kwa sasa biashara hiyo imeshika nafasi katika maeneo mbalimbali ya Jiji la Mwanza hususani maeneo ya vyuoni ikifanywa kwa rejareja na vijana waliohitimu vyuo vikuu mbalimbali nchini.

Njia zinazotumiwa na vijana hao ni pamoja na kuzungusha bidhaa zao yakiwamo matunda kwenye ofisi mbalimbali kwa kutumia toroli ndogo huku wengine wakiuyauza.

Katika Chuo Kikuu cha Mtakatifu Agustino (SAUT) jijini Mwanza, vijana wengi wameamua kujikita katika shughuli hiyo wakati wakisubiri kupata nafasi za ajira endapo zitatokea.

Lakius Hamis (29) alihitimu shahada ya kwanza mwaka 2020 na kuamua kuanza biashara ya matunda katika moja ya mitaa iliyopo karibu na chuo hicho.

Msomi huyo akizungumza na Nipashe, alisema baada ya kumaliza masomo yake hali ilikuwa ngumu na aliamua kuanzisha biashara hiyo ya matunda kwa mtaji wa Sh. 130,000.

Alisema fedha alizipata akiwa chuoni hapo kutoka kwenye fedha za mikopo wanazopewa kwa ajili ya kujikimu (Boom).

Hamis alisema kila siku asubuhi anakwenda sokoni katika soko lililopo eneo la Buhongwa wilayani Nyamagana mkoani Mwanza kununua matunda ambayo huyaandaa na kuyauza mitaani. Aliongeza kuwa baada ya kumaliza chuo aliamua kujiajiri ili asirudi nyumbani kwao jijini Mbeya kwa wazazi wake kwa madai kwamba angekwenda kuwa mzigo.

Msomi huyo alisema mpaka sasa amejenga kibanda cha kuuzia matunda, mboga za majani pamoja na viungo vingine vya mapishi.

"Ninao uhakika wa kupata faida ya Sh. 10,000 kwa siku na naweza kulipia chumba na bado natunza hela ili ninunue kiwanja hapa Mwanza ili niachane na maisha ya kupanga ambapo vyumba vya huku karibu na chuoni bei zipo juu," alisema.

Hamis ambaye ana shahada ya kwanza ya ualimu, alisema kurudi nyumbani baada ya kumaliza chuo bila kazi ni sawa na mchezaji wa mpira kurudisha mpira kwa golikipa jambalo hawezi kulifanya.

Godfrey Chubwa (28) baada ya kuhitimu shahada ya uandishi wa habari na kuamua kujitolea katika redio moja mkoani Mwanza kwa mwaka mmoja bila mafanikio ya ajira, naye aliamua kujiajiri katika biashara ya matunda. "Sina muda mrefu katika biashara hii, lakini hii naiona bora kuliko kukaa sehemu ambapo sipati hata senti tano na bado unaendelea kutumikia, wakati nasubiri ajira ni bora niendelee kutafuta hela ya kujikimu kupitia toroli langu," alisema.

Naye Evodia Jonas (30) yeye ni mhitimu wa shahada ya uongozi wa biashara kutoka Chuo cha Elimu ya Biashara (CBE), anauza matunda mchanganyiko.

Alisema anasambaza matunda katika maduka na ofisi mbalimbali katika Jiji la Mwanza, biashara ambayo alisema inampatia fedha za kujikimu.

"Mpaka sasa ni mwaka wa tatu nimekuwa nikiuza matunda kwa wateja wangu katika ofisi mbalimbali pamoja na maduka na ninapata faida kubwa siwazi tena suala la kuomba ajira," alisema.

Evodia alieleza kuwa ili ufanye hivyo vizuri lazima uzingatie suala la usafi ili uweze kupata wateja wengi, lakini mtu akiwa mchafu pamoja na biashara zake hawezi kuuza. Alisema kazi hiyo imemsaidia kununua kiwanja maeneo ya Buswelu na kumsaidia mama yake.

Msomi huyo alisema anakumbana na vikwazo vingi ikiwamo wanaume kumtaka kimapenzi ili wanunue bidhaa zake na kwamba anapambana navyo ili kuvishinda.

Aliwaomba vijana wengine waliohitimu elimu ya vyuo vikuu sehemu tofauti nchini kuacha tabia za kurudi nyumbani kwao kwa kisingizio cha kukosa ajira mjini.




Wananchi wakiangalia ajali iliyohusisha magari mawili na bajaji katika Barabara ya Goba, eneo la Mbezi Shule, Manispaa ya Ubungo, mkoani Dar es Salaam juzi. **PICHA: SABATO KASIKA**

# CAG abaini upigaji mabilioni ujenzi hospitali

**Na Mary Geofrey**

RIPOTI ya Mkaguzi na Mdhibiti Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) Zanzibar, imebaini ubadhirifu wa fedha katika mradi wa ujenzi wa jengo la mama na mtoto la Hospitali ya Chake Chake, Pemba.

Katika ripoti hiyo, CAG Dk. Othman Abbas Alli amesema kumekuwa na ongezeko la Sh. bilioni 1.3 kutoka Sh. bilioni 2.3 zilizopangwa awali, hivyo kufanya gharama za mradi kuwa Sh. bilioni 3.7.

Pamoja na ongezeko hilo la gharama kwa asilimia 53.7, mradi huo haujakamilika kwa wakati kama ilivyopangwa.

Lengo la mradi huo unaotekelezwa kwa fedha za serikali kwa asilimia 100 ni kupunguza changamoto ya ufinyu wa nafasi kwa watu wanaopata huduma ya mama na mtoto.

Katika utekelezaji wa mradi huo, alisema Wizara ya Afya ilitia saini mkataba wenye kumbukumbu namba SMZ/HOI/W/NCB/W/2018/2019/13 Septemba 17, 2019 na kampuni ya ujenzi ya RANS Company Limited wa Sh. bilioni 1.4 pamoja na kodi ya ongezeko la thamani (VAT) miezi 12 kuanzia Juni Mosi, 2020 hadi Juni Mosi, 2021 lakini ripoti inaonyesha hadi Juni, mwaka jana, ujenzi haukukamilika.

Kwa mujibu wa barua yenye kumbukumbu namba R/MOH/NCHP/04 ya Novemba 21, 2019, mradi wa nyongeza ulikuwa wa Sh. milioni 982 na kusababisha jumla ya gharama ya ujenzi kufikia Sh. bilioni 2.4 sawa na asilimia 67.75.

Kupitia ripoti hiyo, Dk. Othman alionyesha kuwapo kwa ongezeko la gharama za ziada za mradi na kasoro mbalimbali zenye viashiria vya ubadhirifu.

Ripoti hiyo ilieleza kwa kina kuwa ongezeko la gharama ya kazi za ziada zilizowasilishwa kwa mujibu wa barua yenye kumbukumbu namba R/MOH/CMCH/16 ya Julai 29, 2021 ya mkandarasi kwenda kwa mshauri elekezi, ilikuwa na ongezeko hilo la fedha.

Kutokana na kuwapo kwa ongezeko hilo, ilibainika ukiukwaji wa sheria ya ununuzi kwa mujibu wa kifungu namba 49(4-5) cha kanuni ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma ya mwaka 2021.

"Kifungu hiki kinaeleza kwamba iwapo malipo yatazidi bei ya mkataba zaidi ya asilimia 15, yawasilishwe kwa mlipaji Mkuu wa Serikali kwa ajili ya kupata uthibitisho au Baraza la Wawakilishi lakini ukaguzi haukupatiwa uthibitisho huo," alisema CAG.

Kwa mujibu wa CAG, hawakuzingatia pia kuongezeka kwa asilimia 25 ya thamani ya zabuni ya awali, hivyo kusababisha baadhi ya vitu ambavyo havikuwamo kwenye mchoro kufikia Sh. bilioni 2.3 sawa na ongezeko la asilimia 157.86.

Alisema walibaini kutokulipwa kwa fedha za Mshauri Elekezi Sh. milioni 25.7 kwa mujibu wa makubaliano ya mkataba baina ya Wizara ya Afya na Mshauri elekezi ambaye ni msimamizi wa jengo hilo na makubaliano ya gharama ya usimamizi wa ujenzi huo ni Sh. milioni 36.7 ambazo zilitakiwa kulipwa kwa awamu tofauti.

Pia alisema ukaguzi ulibaini kuwa Wizara ya Afya haikutayarisha na kuwasilisha taarifa za matumizi zinazohusiana na utekelezaji wa mradi huo kwa lengo la kukaguliwa na kutolewa ushauri wa kitaalamu.

"Hadi ukaguzi unakamilika, taarifa hizo hazikuwasilishwa jambo ambalo limenyima fursa ya kufahamu fedha halisi iliyopatikana na kutumika katika shughuli za uendeshaji na utekelezaji wa mradi huo," alisema.

# Mshtakiwa wa mauaji adai kubambikiwa kesi na polisi

**Na Grace Gurisha**

MSHTAKIWA Said Abbas (52), ameieleza Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu kwamba, kesi ya mauaji inayomkabili ni zao la polisi la kuwa na roho mbaya na kutumia madaraka vibaya na kwamba yeye hahusiki na mashtaka hayo.

Amedai kuwa, kesi hiyo imetokana na polisi kumkamata wakihisi kuwa ana uhusiano na mfanyabiashara mwenzake Magreth Mwanga, ambaye anaonekana ana uhusiano na mmoja wa askari waliomkamata.

Abbas, alidai hayo jana mbele ya Hakimu Mkazi Mkuu Joyce Minde, wakati akitoa utetezi wake dhidi ya kesi ya mauaji inayomkabili. Abbas anadaiwa kumuua Novatus Busanya akiwa na wenzake wawili.

Akiongozwa na Wakili wake, Godfrey Kizito, Abbas alidai kwamba Agosti 17, 2015 alikamatwa na watu ambao hakuwafahamu kama ni askari polisi baada ya kufikishwa kituo cha polisi.

Alidai kwamba, walimfunga pingu miguuni na mikoni wakamning'iniza kama popo na kuanza kumuuliza kama anamfahamu Mwanga na akadai anamfahamu, ndipo wakaanza kumpiga na kumuuliza kama ana uhusiano naye wa kimapenzi.

Abbas, alidai hana uhusiano naye bali ni mfanyabiashara mwenzake, wakamwambia kama anashirikiana naye kimapenzi atasema tu kwa sababu yuko ndani ya chumba cha 'Yamoto Band' , kwa hiyo atasema tu.

"Baada ya kuona kipigo kinazidi nikakubali kwamba namtaka kimapenzi lakini sijawahi kufanya naye chochote. Nilikuwa sijui kama Mwanga anatoka na askari polisi. Nahisi nilikamatwa kwa sababu wanahisi mimi natembea naye," alidai Abbas.

Pia, alidai kwamba hukuwahi kuhojiwa kuhusiana na tuhuma za mauaji bali ni kuhusu majina yake, sehemu anayoishi na kazi anayofanya, kwa hiyo maelezo wanayodai ameyatoa hakuyatoa na hayajui.

"Mimi najua kusoma na kuandika kwa nini nimeweke saini ya dole gumba wakati najua kuweka sahihi yangu? Hawa walikuwa na nia ovu ndiyo maana wakafanya hivi," alidai.

Kuhusiana na washitakiwa wenzake Idd Mussa na Lutofyo ambao wanashtakiwa naye katika kesi hiyo. Alidai hawatambui bali alionana nao Oktoba 5, 2015 katika Mahakama ya Wilaya ya Kinondoni waliposomewa mashtaka hayo kwa mara ya kwanza. Inadaiwa kwamba Oktoba 14,2015 maeneo ya Changanyikeni ndani ya Wilaya Kinondoni, Dar es Salaam wanatumiwa kumuua Novatus Busanya.

# Kikosi kazi kudhibiti usafirishaji binadamu

**Na Thobias Mwanakatwe,** SINGIDA

SERIKALI imeanza kuchukua hatua kali za kuthibiti biashara ya usafirishaji wa binadamu kwa kuanzisha kikosi kazi maalum ili kuziongezea nguvu taasisi zinazojihusisha na udhibiti wa biashara hiyo haramu.

Ofisa Mwandamizi Sekretarieti ya Kuzuia na Kupambana na Usafirishaji haramu wa binadamu kutoka Wizara ya Mambo ya Ndani na Nchi, Ahmad Mwendadi, alisema hayo juzi wakati wa warsha kwa maofisa wa Polisi, Uhamiaji, Waendesha Mashtaka, Mahakimu na Maofisa Ustawi wa Jamii inayofanyika mjini hapa.

Mafunzo hayo ambayo yanaendeshwa na Shirika la Tanzania Relief Initiatives (TRI), kwa ufadhili wa ubalozi wa Canada nchini, yana lengo la kuwajengea uwezo maofisa hao namna ya kukabiliana na makosa ya usafirishaji wa binadamu.

Alisema kimsingi mikoa yote nchini haiko salama katika suala la biashara ya usafirishaji haramu wa binadamu na kwamba, Tanzania haijakataza mtu kwenda kufanya kazi nje ya nchi lakini kinachotakiwa ni kufuata sheria na taratibu zilizowekwa na serikali.

Mwendadi alisema katika kukabiliana na tatizo hilo, mwaka jana serikali iliwasilisha mswada bungeni kufanya marekebisho ya sheria na kuongeza kosa la kutenda uhalifu kwa kitendo chochote kilichofanywa nje ya sheria.

Hatua nyingine zilizochukuliwa na serikali ni mwaka jana kampuni zote ambazo zilikuwa zikifanya kazi ya kuwatafutia kazi Watanzania nje ya nchi, zilinyang'anywa leseni kwa sababu Watanzania walikuwa wanakumbana na mateso na udhalilishaji huku kampuni hizo zikiwa hazifuatilii.

Mkurugenzi Mtendaji wa TRI, Edwin Mugambila, alisema tatizo la usafirishaji binadamu limekuwa janga la dunia ambapo mamia ya wanawake na watoto wanasafirishwa kupelekwa mijini na nje ya nchi.

Mugambika alisema, tatizo hilo ambalo limeathiri mikoa mingi nchini, wanaosafirishwa kwa kisingizio cha kupewa kazi za ndani lakini wakipelekwa huko wanatumikishwa kingono na kazi zingine ambazo hazizingatii utu na sheria za ajira. Alisema, biashara ya usafirishaji haramu wa binadamu imekuwa ikishamiri nchini kwasababu kulikuwa na udhaifu wa kisheria ambayo inatoa adhabu inayojitosheleza.

"Mtu anafanya kosa na tunaona hii ni biashara kubwa ambayo inatengeneza Dola za Marekani bilioni 150 kwa mwaka lakini mtu anapelekwa mahakamani anatozwa faini Sh. milioni tano au kifungo cha miaka mitano hadi 10," alisema.

Kamanda wa Polisi Mikoa wa Singida, Stellah Rutahibirwa, akifungua warsha hiyo, alitaka ushirikiano baina ya Idara ya Uhamiaji, Ustawi wa Jamii na Jeshi la Polisi kitengo cha Dawati la jinsia ili kuthibiti vitendo vya biashara haramu ya usafirishaji wa binadamu.

Alisema, Idara ya Uhamiaji kabla ya kutoa hati za kusafiria kwa watoto wenye umri kati ya miaka 12-13, iwe inajiridhisha kwa sababu watoto wa umri huo ndio wamekuwa wakipelekwa kwenda kutumikishwa na kufanyiwa vitendo vya kikatili.



Madaktari wa upasuaji wa kurekebisha viungo 'plastic surgery' kutoka nchini Uingereza, wakiwa kwenye wodi ya watoto ya Hospitali ya Taifa ya Muhimbili (MNH), jijini Dar es Salaam jana, walipokwenda kuzungumza na wenzao wa hospitali hiyo kuhusu kuanzisha ushirikiano wa matibabu. **PICHA: JOSEPH MWENDAPOLE**

# Madaktari bingwa kutoka Uingereza wafanya upasuaji wagonjwa, majeraha

**Na Joseph Mwendapole**

WATAALAMU sita wa upasuaji wa kurekebisha viungo kutoka Uingereza, wako nchini na tayari wamewatibu wagonjwa wanane kwa kurekebisha majeraha waliyokuwa nayo.

Madaktari hao ni Naveen Cavale, kutoka Hospitali ya Kings College, Foiz Ahmed kutoka Hospitali ya Lister Stevanage na Asmat Din kutoka Hospitali ya St Thomas jijini London.

Wengine ambao ni madaktari walioko kwenye mafunzo ni Mezika Moghim, kutoka Hospitali ya Royal Free ya London, Terouz Pasha kutoka Hospitali ya Mtakatifu Thomas na Emma Murray kutoka Hospitali ya Alder Hey Children ya Liverpool.

Mabingwa hao waliwasili nchini wiki iliyopita na wamekuwa wakiwafanyia upasuaji wagonjwa hao kwenye Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Pwani ya Tumbi, mjini Kibaha. Mkuu wa ujumbe wa wataalamu hao, Dk. Naveen Cavale, alisema wamekuwa wakifika nchini mara mbili kwa mwaka kwa ajili ya kazi hiyo.

Alisema, wamekuwa wakitoa mafunzo hayo ya kitaalamu kwa wakufunzi wa Tanzania kwa kushirikiana na hospitali mbalimbali lengo ikiwa ni kuwaongezea ujuzi.

"Tumekuwa tukirekebisha ngozi zilizoharibiwa na majeraha ya moto na matatizo mengine ambayo watoto wamezaliwa nayo. Tumekuja Muhimbili kuangalia namna ya kushirikiana kutoa mafunzo kwa wataalamu wake," alisema.

Alisema, mbali na Muhimbili, wako kwenye mazungumzo na baadhi ya hospitali za rufani za kanda ili kuanzisha ushirikiano wa kufanya upasuaji wa aina hiyo.

"Tumefanya upasuaji wa watu wote hao kwenye hospitali ya Tumbi na wakati mwingine tukija tunatarajia kufanya hapa Muhimbili na hospitali za Arusha na kwingine. Kokote tutakakoitwa kutoa huduma hii tutafika kusaidia," alisema.

Dk. Cavale, alisema wanatarajia kurudi nchini kila baada ya miezi sita kufanya upasuaji wa aina hiyo na watakapopata wataalamu wengi, watakuwa wanakuja kila baada ya miezi miwili.

Akizungumza kuhusu namna ya kuwasaidia kimafunzo wataalamu wa ndani, Dk. Cavale alisema mafunzo kwa madaktari wa upasuaji wa aina hiyo yanachukua hadi miaka sita Uingereza na miaka minne kwa Tanzania.

"Mafunzo kama haya yanachukua muda mrefu sana lakini tutashirikiana na mashirika mengine kama COSECSA, ambalo linatoa mafunzo kama haya kwa ukanda wa kusini mwa jangwa la Sahara.

"Kupitia shirika kama COSECSA tunatarajia kuanzisha mafunzo hapa nchini kama yale tuliyonayo nchini Uingereza na kwa kufanya hivyo kwa miaka michache ijayo tunaamini tutazalisha wataalamu wengi wa fani hii," alisema Dk. Cavale

Naye Dk. Foiz Ahmed, kutoka Hospitali ya Lister Kaskazini mwa London, alisema matatizo mengi waliyokutana ni kuungua kwa watoto mikononi na miguuni.

Alisema, wamekuja nchini kwa mwamvuli wa shirika la kujitolea la British Foundation for International Reconstructive Surgical Trainings .

"Sisi tulikuja hapa kuwapa mafunzo wakufunzi wa hapa nchini ili waweze kufanya upasuaji kama huu kwasababu peke yetu hatuwezi kuwafanyia wagonjwa wengi lakini tukiwapa mafunzo watawafanyia upasuaji wagonjwa wengi," alisema.

Dk. Foiz alisema shirika hilo la kujitolea liko chini ya umoja wa wataalamu wa kurekebisha viungo nchini Uingereza na wana miradi ya aina hiyo nchini Bangladesh, Cambodia, Malawi na wanatarajia kuanzisha Tanzania.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Kuachwa wakongwe Stars iwe fundisho kwa chipukizi

**WAKATI** hatua ya awali ya mashindano ya kimataifa ya Ligi ya Mabingwa na Kombe la Shirikisho ambayo husimamiwa na Shirikisho la Soka Afrika (CAF), inakamilika wikendi hii kwa timu sita za Tanzania kushuka dimbani, kikosi cha Timu ya Taifa (Taifa Stars), kimeitwa kwa ajili ya kujiandaa na mechi mbili za kimataifa.

Mechi hizo za kirafiki za kimataifa zitachezwa katika kalenda rasmi inayotambulika na Shirikisho la Soka la Kimataifa (FIFA), na Taifa Stars inatarajia kucheza dhidi ya majirani zao, Uganda (Cranes) na Waarabu wa Libya. Ili kupata wachezaji kwa ajili ya kuitumikia Stars, ni lazima mchezaji uonyeshe kiwango kizuri katika mechi za mashindano yote ndani ya klabu yako, mchezaji unatakiwa utoe mchango kwa timu yao ili ifikie malengo iliyojiwekea katika msimu husika.

Kwa hapa nchini, wachezaji wa Tanzania watatakiwa kufanya vyema kupitia mashindano ya Ligi ya Mabingwa Afrika ambayo Simba na Yanga zote za jijini Dar es Salaam zinashiriki, sawa na wanaochezea KMKM ya Zanzibar. Kwa upande wa mashindano ya Kombe la Shirikisho Afrika, Azam FC ya jijini pia, Geita Gold FC kutoka mkoani Geita na Kipanga ya Zanzibar, wachezaji wake wanatakiwa kujituma ili kuwashawishi makocha wa Stars kuwaita kwenye kikosi chao.

Hakuna jambo lisilojificha kuwa mchezaji mwenye kiwango bora katika klabu yake ndio anayepata nafasi nzuri ya kuitwa kuvaa jezi ya taifa lake, hii haitaji kufanya mahesabu makali kama ya kuchanganya kemikali.

Katika kuhakikisha Stars inafikia malengo yake ya kufanya vizuri katika mashindano mbalimbali inayoshiriki na si kusindikiza mataifa mengine, ni lazima iite wachezaji wanaoonyesha viwango vya juu kwenye klabu zao.

Na hii si tu Stars inapokabiliwa na mechi za mashindano, hata pale inapokuwa na michezo ya kirafiki kwa sababu inapoibuka na ushindi, husaidia kuipa nchi pointi na hivyo kupanda kwenye orodha ya viwango vya ubora vinavyotolewa na FIFA kila baada ya miezi mitatu.

Hongera Kaimu Kocha Mkuu wa Stars, Honour Janza, kwa kuthubutu kuwaacha wachezaji waliokuwa wamezoeleka au wamejijengea himaya katika timu hiyo ili kuanzisha safari mpya ya matumaini ambayo imekuwa ni kiu cha muda mrefu cha Watanzania.

Mzambia huyo ameamua kuwaweka pembeni nyota kadhaa akiwamo nahodha wa mabingwa watetezi wa Ligi Kuu Tanzania Bara, Yanga, Bakari Mwamnyeto, kiungo, Farid Mussa, Salum Aboubakari (Yanga), Jonas Mkude na Mohamed Hussein maarufu Zimbwe Jr na kuwaipa nyota wapya ili kuona timu hiyo inafika kule inapokuhitaji.

Inawezekana wachezaji hao wameachwa kwa sababu ya kushuka viwango vyao au hawajitumi kama ilivyotarajiwa na sasa nafasi wamepewa wachezaji wengine chipukizi au ambao wana uzoefu lakini walikosa namba kutokana na kushindwa kupambana na wakongwe hao.

Tunaamini wachezaji wapya walioitwa katika timu hiyo wanatakiwa kuonyesha bidii na juhudi kwa ajili ya taifa lao pia kutumia nafasi waliyoipata kujitangaza na hatimaye kujiongezea thamani.

Ni jambo lisilofichika mchezaji anapoonyesha kiwango bora ndani ya Stars anakuwa amejiweka katika daraja zuri atakaporejea kwenye klabu yake, lakini atazivutia timu nyingine mara dirisha la usajili litakapofunguliwa katika msimu unaofuata.


Lakini tunawakumbusha wale ambao wameachwa katika kikosi hicho kuendelea kupambana na hatimaye kurudi katika kikosi hicho kwa faida ya nchi na wao binafsi, wasikate tamaa kwamba wamekwisha, waamini timu ya taifa ni ya kila mtu na utaitwa pale tu kiwango chako kitakapokuwa kimelivutia benchi la ufundi na si vinginevyo.

Kufanya vizuri kwa Stars kutasaidia kuzivutia kampuni na taasisi nyingine mbalimbali kuwekeza katika mchezo huo pia kumpa heshima Rais Samia Suluhu Hassan, ambaye ameongeza bajeti katika mchezo huo wa soka na mingine. Kwa sasa wachezaji wa Stars wanapata huduma bora zinazostahili, nao imefika wakati wakurudisha furaha hiyo kwa Watanzania kwa kupambana kusaka matokeo bora, ingawa inafahamika katika soka kuna matokeo ya aina tatu. Bila kusahau kuwatakia kila la heri wawakilishi wa Tanzania katika michuano hiyo ya CAF ambao wanakamilisha mechi za hatua ya awali kwa kumaliza vyema na kusonga mbele.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:

**THE GUARDIAN LIMITED**

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






## Muungwana Lazima Nilonge

# Simba, Yanga, Geita kazi CAF haijamalizika

Na Adam Fungamwango

**MABINGWA** watetezi wa Ligi Kuu Tanzania Bara,Yanga leo usiku watakuwa kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa kucheza mechi ya Ligi ya Mabingwa Afrika dhidi ya Zalan FC ya Sudan Kusini, huku wawakilishi wengine katika michuano ya Kombe la Shirikisho, Geita Gold wao wakiivaa Hilal Alsahili kwenye Uwanja wa Azam Complex.

Simba, kesho nayo itakuwa dimbani katika mechi ya Ligi ya Mabingwa Afrika dhidi ya Nyasa Big Bullets kutoka Malawi.

Mechi zote ni marudiano ya michuano hiyo ya kimataifa, Yanga ikishinda mabao 4-0 kwenye mechi ya kwanza iliyochezwa hapa hapa nchini, Simba ikishinda magoli 2-0 ugenini Malawi, na Geita Gold ikipoteza kwa bao 1-0 huko Sudan.

Ukiangalia hapa kwa kiasi kikubwa ni kwamba timu za Tanzania zipo katika mazingira mazuri ya kusonga mbele kwenye hatua ya raundi ya kwanza ya michuano hiyo ya kimataifa.

Binafsi ninaziombea timu zote za Tanzania zifanye vyema kwenye michuano hiyo kwa sababu itakuwa ni faida kubwa wa soka la Tanzania. Tukianza katika Ligi ya Mabingwa Afrika kama Simba na Yanga zitavuka hatua hii, ina maana zina uhakika wa kuendelea tena mbele.

Kwa sababu kama zitashinda kwenye mechi za raundi ya kwanza, zitaingia kwenye hatua ya makundi ya Ligi ya Mabingwa Afrika.

Yanga kama itapita itasubiri mshindi kati ya St George ya Ethiopia na Al Hilal ya Sudan, huku Simba kama itaitoa Nyasa Big Bullets, itasubiri mbabe wa mechi kati ya Red Arrows ya Zambia na Primeiro de Agosto ya Angola.

Lakini pia kama zitatolewa kwenye hatua hii ya raundi ya kwanza, zitashuka kwenye michuano ya Kombe la Shirikisho Barani Afrika kwenda kwenye hatua ya mchujo, kutafuta kutinga hatua ya makundi ya kombe hilo.

Hii inaonyesha kazi kubwa ambayo Simba na Yanga zinatakiwa kufanya kwanza ni kupita kwenye hatua hii kwanza.

Yoyote itakayotolewa hapa, ni kwamba itabidi kusubiri tena mwakani na si vinginevyo.

Hivi karibuni Rais wa Shirikisho la Soka Nchini (TFF), Wallace Karia alisema anachotaka safari hii ni kuona timu za Tanzania zinafanya vema kwenye michuano ya kimataifa ili kuzilinda nafasi nne za uwakilishi.

Kwa miaka ya hivi karibuni tumeona Tanzania ikitoa wawakilishi wawili, bingwa na mshindi wa pili kucheza Ligi ya Mabingwa, mshindi wa tatu na bingwa wa Kombe la FA wanaopata tiketio ya kucheza Kombe la Shirikisho.

Tanzania imeipita mpaka Zambia, nchi ambayo ina historia kubwa kwenye soka, lakini mwaka huu inatoa mwakilishi mmoja tu kwenye Ligi ya Mabingwa na mshindi wa pili anayecheza Kombe la Shirikisho.

Kwa sababu hiyo ni lazima Karia atoa rai ya kuzilinda nafasi hizo ili Tanzania isirudi tena nyuma kwa sababu zinapatikana kutokana na timu zinazoshiriki kufanya vizuri.

Imefika wakati sasa Watanzania kuacha mambo yaliyopitwa na wakati ya kuwasaidia wageni ili kuifunga timu mwenyeji.

Tumekuwa tukiona huko nyuma, viashiria vya baadhi ya timu kuzipokea timu pinzani zinazocheza na timu za hapa hapa, kwa sababu tu ya kisingizio cha utani wa jadi, hii si sahihi kabisa.Mbali na hilo, tumekuwa tukiona baadhi ya viongozi wa klabu hapa nchini wakitoa mbinu kwa wageni jinsi gani ya kufanya ili kuepuka kufungwa kwa kile wanachodai kuwafundisha kuepuka hujuma.

Kwenye soka la kisasa haya mambo hayana nafasi. Cha ajabu ni kwamba huko nyuma hakukuwa na vitu kama hivyo.

Yanga ikicheza mechi ya kimataifa, mashabiki wa Simba watakwenda tu kutazama, kupongeza kama wenzao watashinda na kuwazodoa kama wakifungwa. Na upande wa pili ni hivyo hivyo. Lakini hatukuona timu zikifanyiana hujuma, mmoja ufungwe ili asimcheke mwenzake.

Hili limeanza kwenye miaka ya karibuni kwenye kipindi ambacho tunadhani soka likua kuliko zamani. Inashikitisha sana.

Ifike wakati sasa kila timu iangalie mechi zake, inacheza, inashindaje na inasongaje mbele, badala ya kutumia nguvu nyingi kutaka kuhujumu mechi za kimataifa za timu nyingine.

Nadhani kufanya hivi ni sawa tu na kuhujumu maendeleo ya soka la Tanzania na nchi kwa ujumla kwa sababu kama timu hizi zikisonga mbele licha ya nchi kupata sifa, lakini kuna vitu vingi ambavyo nchi inanufaika navyo pamoja na Shirikisho la Soka Nchini.

Klabu ziwe na wivu wa maendeleo kuangalia zingine zimefanya nini na kupita wapi ili zifuate, na siyo kutaka kuzishusha kwa mtindo wa 'tukose wote'.

Narudia tena kutoa rai kama ile ya Karia kuzitakiwa timu zote kila la heri, lakini kuacha tabia ya kuhujuliama kwa sababu siyo kama inasababisha timu hiyo kufungwa tu, lakini pia inadumaza soka la Tanzania kwa kuonekana timu zake labda si imara, kumbe kuna mchezo mchafu unafanywa wa kudhoofisha nguvu ya timu zingine kwenye mechi za kimataifa.

Kama ikitokea, TFF ilichukulie hili kama hujuma kwa soka la Tanzania.

HABARI BUNGENI

# Mbunge ataka mapitio ya upimaji vijiji nchini

MBUNGE wa Liwale (CCM), Zuberi Kuchauka, ameitaka serikali kufanya mapitio ya upimaji wa vijiji kote nchini kwa kuwa migogoro mingi imesababishwa na upimaji usio shirikishi wa mwaka 1970.

"Kuna mgogoro Kilwa na Liwale katika kijiji cha Nanjilinji unafanana na huu, wakati wa upimaji wakazi hawa wa wilaya mbili hawakushirikishwa," alisema.

Akijibu maswali hayo, Naibu Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Ridhiwani Kikwete, alikiri kuwapo na maeneo yenye migogoro ya aina hiyo.

Aidha, alisema kilichofanyika katika miaka ya 1970 haikuwa upimaji wa vijiji bali ilikuwa operesheni maalum ya serikali ya kuanzisha vijiji vya ujamaa nchini.

"Miaka ya 2000 serikali ilitekeleza Programu ya Upimaji wa Vijiji kwa lengo la kuvifanya kuwa mamlaka kamili za usimamzi wa ardhi ya kijiji," alisema.

Naibu Waziri alibainisha kuwa mkoa wa Lindi, vijiji 401 kati ya 523 vikiwamo vya wilaya ya Liwale vimepimwa kwa njia shirikishi na kuwekewa alama za mipaka.

"Natambua kumekuwapo na changamoto tangu programu hiyo ilipoanza kutekelezwa. Aidha, kuna umuhimu wa kufanya mapitio ya upimaji wa vijiji kwa njia shirikishi hasa kwa vijiji ambavyo upimaji wa mipaka yake unalalamikiwa," alisema.

Hata hivyo, alisema wizara kwa kushirikiana na mamlaka zingine imeendelea kufanya mapitio ya kuboresha mipaka ya vijiji ilivyovipima nchi nzima ili kuondoa changamoto za migogoro ya mipaka.

Pia, alisema katika kipindi cha miaka mitano 2022/23 hadi 2026/27, Wizara imepanga kufanya mapitio ya upimaji wa vijiji 250 vyenye tatizo la mipaka kupitia Mradi wa Kuimarisha Milki za Ardhi (LTIP)

"Natoa rai kwa mamlaka za upangaji kutenga fedha katika bajeti zao kwa ajili ya kufanya mapitio ya mipaka ya vijiji katika halmashauri zao kwa njia shirikishi ili kupunguza migogoro," alisema.

# Waziri awatoa hofu wananchi madai ya samaki kuhifadhiwa maji ya maiti

WIZARA ya Mifugo na Uvuvi, imewatoa hofu na kuwahakikishia Watanzania kuwa samaki wanaovuliwa na kupelekwa katika masoko mbalimbali ni salama na hawawekwi maji ya maiti.

Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Abdallah Ulega, aliyasema hayo bungeni jana alipokuwa akijibu swali la nyongeza la Mbunge wa Viti Maalum (CHADEMA), Cecilia Pareso.

Katika swali lake, Pareso alisema kumekuwa na taarifa katika vyombo vya habari kuwa uhifadhi wa samaki katika baadhi ya maeneo nchini, unafanywa kwa kutumia dawa za kuhifadhia maiti, jambo ambalo limesababisha taharuki kwa wananchi.

"Wananchi hawafahamu wafanye nini ili wasipate hao samaki waliohifadhiwa kwa namna hiyo. Je, nini mkakati wa serikali wa kuhakikisha samaki hao hawahifadhiwi kwa vitu hivyo vinavyosababisha kansa kwa Watanzania?" alihoji.

Akijibu swali hilo, Naibu Waziri Ulega alisema jambo hilo halina hakika na kwamba hadi hivi sasa watu wanahisia kwamba kiko kitu cha namna hiyo.

"Ndiyo maana Makamu wa Rais, Dk. Philip Mpango, alipokuwa jijini Mwanza, aliagiza Wizara ya Afya ifanye utafiti ili kama ni kweli kinafanyika kitu kama hicho kizuiwe mara moja.

" Nawaomba niwatoe hofu Watanzania hakuna jambo kama hilo. Tuchukue samaki kutoka Mwanza tulete Dodoma au tupeleke Dar es Salaam kwa kuhifadhi na maji ya maiti? Haliko jambo la namna hiyo,"alisema.

Alisisitiza Watanzania wawe na uhakika samaki wanaovuliwa na wavuvi na wanaokwenda katika masoko mbalimbali wako salama na kwamba hawana shaka yoyote.

Katika swali la msingi, Mbunge wa Sengerema (CCM), Hamis Tabasamu, alihoji lini ujenzi wa banda la ukaguzi wa kupokelea samaki wabichi katika Kata ya Chifunfu utakamilika.

Akijibu swali hilo, Ulega alisema ujenzi wa banda la kupokelea samaki la Chifunfu wilayani Sengerema ulianza Mei, 2021 chini ya M/S Fast Construction Co. Ltd ya mkoani Mwanza kwa thamani ya Sh. milioni 124.59 na hadi sasa ujenzi umefikia hatua ya kuezeka na na kwamba mkandarasi amelipwa Sh. milioni 95.7.

"Kazi ya ujenzi wa banda hilo ilipangwa kukamilika ndani ya miezi sita. Hata hivyo mkandarasi hakukamilisha kazi hiyo kwa mujibu wa mkataba, hivyo serikali imechukua hatua za kusitisha mkataba wa mkandarasi huyo na hatua zingine za kisheria zinaendelea dhidi yake," alisema.



Spika wa Bunge, Dk. Tulia Ackson (kushoto), akijadiliana jambo na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge na Uratibu, George Simbachawene, Bungeni jijini Dodoma jana. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Ujenzi zahanati 555 wafikia hatua nzuri

SERIKALI imesema zaidi ya asilimia 85 ya maboma ya zahanati 555 nchini yaliyopelekewa fedha kwa mwaka 2021/22, yamekamilika.

Naibu Waziri wa Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Dk. Festo Dugange alibainisha hayo jana bungeni alipokuwa akijibu maswali ya nyongeza ya Mbunge wa Meatu (CCM), Leah Komanya.

Katika swali lake, Komanya alihoji serikali haioni haja ya kupeleka mwongozo wa matumizi kwenye fedha za kukamilisha maboma ya zahanati.

"Ni miaka miwili sasa serikali imepeleka fedha. Je, serikali iko tayari kufanya sensa kuangalia fedha zilizopelekwa kukamilisha maboma zinaendana na maboma yaliyokamilishwa?" alihoji.

Akijibu maswali hayo, Dk. Dugange, alisema kila boma lilipata Sh. milioni 50 na asilimia 85 yamekamilika na yapo hatua za mwisho kusajiliwa.

Pia alisema, serikali ilipeleka mwongozo wa namna ambavyo fedha zilizopelekwa kukamilisha maboma ya zahanati Sh. milioni 50 kwa kila boma zinatakiwa kutumika na kukamilisha maboma.

"Pendekezo moja wapo lilikuwa boma ambalo limeombewa Sh. milioni 50 lazima liwe limefika hatua ya lenta sio msingi au chini ya lenta na hesabu zilizofanywa ni kwamba Sh. milioni 50 zikipelekwa kwenye jengo ambalo limefikia hatua ya lenta linakamilika na kuanza kutoa huduma za afya," alisema.

Katika swali la msingi, Komanya alihoji mpango wa serikali wa kukamilisha maboma ya zahanati vijiji vya Lata, Ikigijo, Lukale, Malwilo, Bulyanaga, Shushuni, Nata, Usiulize na Igushilu.

Naibu Waziri Dugange, akijibu swali hilo, alisema serikali katika mwaka wa fedha 2021/22 ilipeleka Sh. milioni 200 katika wilaya ya Meatu kwa ajili ya ukamilishaji wa zahanati nne.

Pia alisema, kwa mwaka 2022/23, serikali imetenga Sh. milioni 200 kutoka serikali kuu na Sh. milioni 100 kutoka mapato ya ndani ya halmashauri kwa ajili ya ukamilishaji wa Zahanati za Mwandikisasa, Masanga, Mwanyahina, Mwabagashi na Ikigijo.

"Katika mwaka wa fedha 2023/24 Sh. milioni 100 zitatengwa kutoka mapato ya ndani ya halmashauri kwa ajili ya ukamilishaji wa zahanati za Igushilu na Nata," alisema.




**Na Augusta Njoji, DODOMA**

## CRDB yazindua kampeni maalum elimu bima ya vyombo vya moto

**Na Mwandishi Wetu**

BENKI ya CRDB imezindua kampeni maalum ya elimu ya bima ya vyombo vya moto iliyopewa jina la 'Kuwa Shua', hafla ya uzinduzi huo ilifanyika katika gereji ya MacAuto iliyoko Sinza jijini Dar es Salaam juzi.

Akizungumza na waandishi wa habari wakati wa uzinduzi huo, Mkuu wa Kitengo cha Bima Benki ya CRDB, Moureen Majaliwa alisema lengo la kampeni hiyo ni kuhamasisha wamiliki wa vyombo vya moto kukatia vyombo vyao bima ili kujikinga dhidi ya majanga.

Majaliwa alisema pamoja na kuwa bima ya vyombo vya moto ni moja ya bima zinazotumika kwa kiasi kikubwa, wamiliki wengi wa vyombo vya moto nchini hawana elimu ya kutosha kuhusu bima, jambo linalosababisha wengi kupuuzia.

"Katika kipindi cha kampeni maofisa wetu wa benki watakuwa wakitembelea wateja kuwapa elimu ya bima za vyombo vya moto, pia tutakuwa tukitoa zawadi kwa wateja watakaokata bima kupitia Benki ya CRDB," alisema Majaliwa.

Akitoa ufafanuzi kuhusu zawadi kwa wateja, Majaliwa alisema wamiliki wa vyombo vya moto watakaolipia bima kubwa ya 'comprehensive' watarudishiwa asilimia tano ya kiasi cha bima (kabla ya VAT) kama mafuta kupitia vituo vya Oryx nchi nzima.

"Baada ya kulipia bima, ama kupitia tawi la benki, CRDB Wakala au SimBanking, mbali ya mteja kupokea ujumbe wa sera yake ya bima, pia atapokea ujumbe wenye nambari ya zawadi ambayo ataitumia kujaza mafuta katika vituo vya Oryx," alifafanua.

Taratibu za usalama nchini zinaelekeza kuwekwa sharti la lazima kwa vyombo vya moto kuwa na bima kabla ya kuruhusiwa kuingia barabarani. Majaliwa alisema jamii inapaswa kuchukulia kwa umuhimu huduma hiyo ya bima kujikinga na majanga ya ajali za barabarani.

Majaliwa alisema kampeni hiyo pia inalenga katika kusaidia malengo ya serikali kupitia Mpango wa Maendeleo ya Sekta ya Fedha ya kuongeza ujumuishi wa Watanzania katika huduma za bima kufikia asilimia 50 ifikapo mwaka 2030.

Katika kuhakikisha kuwa kampeni hiyo inakuwa na mafanikio, Benki ya CRDB imeandaa Tamasha la Elimu ya Bima ya Vyombo vya Moto litakalofanyika Viwanja vya Posta, Kijitonyama kesho.

Tamasha hilo linakusudia kuwaleta pamoja wadau mbalimbali wa vyombo vya moto; kampuni za bima, gereji, maduka ya vifaa, Mamlaka ya Usimamizi wa Bima (TIRA), Msuluhishi wa Migogoro ya Bima na Jeshi la Polisi.

Meneja Uendeshaji Huduma za Bima Benki ya CRDB, Tumaini Frank aliwakaribisha wamiliki wa vyombo vya moto kushiriki katika tamasha hilo ili kupata elimu, pia kukutana na watoa huduma mbalimbali.

"Katika tamasha hilo pia kampuni za bima zitakuwa zikishughulikia madai ya wateja, hivyo hii ni nafasi muhimu kwa wale ambao wana madai ambayo hayajafanyiwa kazi." alisema Tumani.

# CBE yasaka bil. 1.2/- bweni la wasichana

**Na Joseph Mwendapole**

CHUO cha Elimu ya Biashara (CBE), kimeandaa harambee ya kukusanya Sh. bilioni 1.2 kwa ajili ya ujenzi wa hosteli za wasichana kwenye kampasi yake jijini Mbeya.

Mkuu wa chuo hicho, Prof. Emmanuel Mjema, alisema hayo jana jijini Dar es Salaam wakati akizungumza na waandishi wa habari kuhusu harambee hiyo yenye kaulimbiu "Changia Zaidi ya Harusi, Uwe Sehemu ya Kuleta Tabasamu kwa Mtoto wa Kike".

Alisema wameamua kuanza na ujenzi wa hosteli za wasichana kutokana na changamoto wanazopata wanapokuwa nje ya kampasi kulinganisha na wavulana.

Alisema kilele cha harambee hiyo inayosimamiwa na mlezi wa kampasi hiyo, Spika wa Bunge, Dk. Tulia Ackson, kitakuwa Septemba 24 jijini Mbeya.

Prof. Mjema alisema wanafunzi wengi wa ngazi ya diploma na cheti bado ni wadogo, hivyo wanahitaji mazingira mazuri ya kusomea ndani ya kampasi hiyo.

"Si kwamba tunawatenga wanafunzi wa kiume bali tunazingatia hali halisi na mazingira yalivyo ndiyo maana tumeamua kuanza na hosteli za wasichana na baadaye tutajenga za wakiume," alisema Prof. Mjema.

Pia alisema chuo kimefanya jitihada za kuwafikia wadau mbalimbali zikiwemo taasisi na mashirika ya serikali, yasiyo ya serikali na sekta binafsi kuomba michango.

"Tumefikisha ombi letu kwa waheshimiwa wabunge ambao ni wadau muhimu wa maendeleo ya elimu na tunawaomba wadau wote wenye mapenzi mema watushike mkono ili tukamilishe jambo letu," alisema

Aliwashukuru wadau mbalimbali ambao wameshachangia ujenzi huo na wengine wametoa ahadi zao kufanikisha ujenzi huo. Aliwataja baadhi yao kuwa ni benki ya NMB, WMA, BRELA, TBS, NHC, St John University, wajumbe wa bodi ya uongozi CBE, wahitimu wa CBE, wanafunzi wasasa na Mkuu wa Mkoa wa Mbeya , Juma Homera ambaye ametoa shilingi 5,000,000.

"Kipekee napenda kumshukuru Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Juma Homera, ambaye kiukweli amekuwa kiongozi anayejitolea kwa hali na mali kuhakikisha jambo hili linafanikiwa. Mkurugenzi wa Mamlaka ya Elimu Tanzania TEA naye amekuwa nasi bega kwa bega kukusanya fedha," alisema.

"Kwa niaba ya mlezi wa kampasi ya Mbeya, Dk. Tulia Ackson tunawakaribisha wadau wote wafike kwenye harambee tarehe 24 mwezi huu kwenye hoteli ya Eden jijini Mbeya kuanzia jioni. Tunaomba wadau wote watakaopata ujumbe huu wasikie kilio chetu tujenge hosteli za wasichana," alisema

Aliwaomba wasamaria wema kuchangia ujenzi huo kupitia akaunti ya NMB 20601100030, TigoPesa 0710 999237 na kupitia akaunti ya M-PESA ambayo ni 0742 135979.



Baadhi ya wakazi wa Jiji la Dar es Salaam, wakiangalia vitabu vya Big Bad Wolf katika maonyesho kwenye ukumbi wa Diamond Jubilee, jijini jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Waliofikiwa elimu ya UVIKO-10 waongezeka

**Na Mary Geofrey**

CHAMA cha Viziwi (CHAVITA), kimesema idadi ya kundi hilo waliopata chanjo ya UVIKO-19 imeongezeka kutoka 87 hadi 303 baada ya kupewa elimu.

CHAVITA kwa kushirikiana na Wizara ya Afya kwa ufadhili wa Shirika la Umoja wa Mataifa la Kuhudumia Watoto (UNICEF), lilitoa elimu ya chanjo kwa kundi hilo katika mikoa ya Arusha, Mwanza na Mbeya.

Mratibu wa Mradi huo wa UNICEF wa kutoa elimu kuhusu UVIKO-19 kutoka CHAVITA, Lupi Mwaisaka, alieleza takwimu hizo jana jijini Dar es Salaam wakati akizungumza na waandishi wa habari kuhusu maadhimisho ya Siku ya Viziwi yatakayofanyika kuanzia Septemba 26 hadi Oktoba Mosi mkoani Mtwara.

Alisema awali viziwi walikuwa hawataki kupata chanjo ya UVIKO-19 kwa kuamini damu itaganda na mambo mengine ya imani potofu.

"Baada ya kupata mradi huu kwa kushirikiana na wizara ya afya na UNICEF tuliwafikia wananchi 42,961 na kuwapa elimu kuhusu umuhimu wa chanjo na hivyo wananchi 216, wakaamua kuchanua," alisema Mwaisaka.

Alitaja wilaya walizofika kutoa elimu ni Arusha Mjini, Meru na Karatu (Arusha) , Ilemela Sengerema, Magu(Mwanza) na Mbeya Mjini na Kyela (Mbeya).

Aliwataka wananchi kuendelea kuchukua tahadhari na kupata chanjo ya UVIKO-19 ili kujikinga na maambukizi.

Kuhusu maadhimisho ya siku ya viziwi, alisema lengo la kuadhimisha siku hiyo ni kutoa mwamko kwa jamii, serikali na wadau wa maendeleo kutambua mahitaji ya viziwi na kuchukua hatua kuwajumuisha ili kuondoa unyanyapaa kwenye jamii.

Alisema kauli mbiu katika maadhimisho hayo ni 'Kujenga Jamii Jumuishi' na mgeni rasmi anatarajiwa kuwa Waziri wa Afya, Ummy Mwalimu na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Innocent Bashungwa.

Awali, Mwenyekiti wa Shirikisho la Watu Wenye Ulemavu (SHIVYAWATA), Ernest Kimaya, alihimiza watu wenye ulemavu kuendelea kujitokeza kupata chanjo ya UVIKO- 19 ili kujikinga na maambukizi.



# Mradi wa visima kupunguza tatizo la maji jiji la Dodoma

**Na Mwandishi Wetu,** DODOMA

KATIKA kukabiliana na upungufu wa maji katika Jiji la Dodoma, Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Dodoma (DUWASA) imeendelea na uchimbaji wa visima pembezoni mwa mji vikiwamo vitano maeneo ya Nzuguni A na B.

Akizungumza katika upimaji wa wingi wa maji Mtaa wa Nzuguni A jijini hapa, Fundi Pampu wa DUWASA, Fadhili Mahonya, alisema kazi inayoendelea kwa sasa ni upimaji wa pampu ili kujua uwezo wa kisima na kupata pampu sahihi itakayotumika.

"Kisima hiki kina urefu wa mita 134 kwenda chini na kina uwezo wa kuzalisha maji lita 65000 kwa saa," alisema.

Naye Mwenyekiti wa Mtaa wa Nzuguni A, Onaeli Mathias, alisema ni muda mrefu sana tangu uhuru eneo la Gogwa na Dundulu kumekuwa na shida ya maji.

"Kwa mradi huu wa DUWASA ni jambo la kushukuru sana, namshukuru Rais na Waziri wa Maji na uongozi wa DUWASA. Kwa kweli hili tatizo lilikuwa sugu tangu uhuru walikuwa wanatumia maji ya kisima," alisema.

Alisema watu wamepata maradhi hasa homa ya matumbo kutokana na kunywa maji yasiyo salama.

"Maji yakipatikana hata eneo hili linaweza kuimarika kwani kwa sasa limekuwa kame sana," alisema.

Nao wananchi wa Nzuguni A waliishukuru Serikali kupitia DUWASA kwa kuwapelekea huduma ya maji katika eneo hilo.

Rehema Simon alisema: "Tunashukuru sana kwa huduma hii maana wanawake tumetuliwa ndoo kichwani kwani tulikuwa tunachota maji mbali huku mtoto akiwa mgongoni.

"Tunamshukuru Mungu na Serikali pia kupitia DUWASA, kwa kutuletea maji, kwani kwa sasa gharama ya kupata maji ni kubwa unalipia maji pamoja na usafiri kwa gharama ya 65,000," alisema.

Mkazi mwingine, Prosper Mnyoli, alisema upatikanaji wa maji utachochea ujenzi kwenye maeneo hayo kwa kuwa awali walikuwa wanatumia gharama kubwa za ujenzi.

"Tulikuwa tunafuata maji kama kilomita nne, lakini kwa maji haya kusogea karibu itakuwa imeturahisishia,"alisema.

Pia alisema kukamilika kwa visima hivyo kutaongeza kiwango cha maji eneo la Nzuguni hivyo kupunguza au kuondoa kero ya maji katika eneo hilo na maeneo ya jirani ikiwamo Ilazo.



Mhandisi wa soko la wazi la Machinga Complex, jijini Dodoma, Ntezimanu Chanyela (wa pili kulia), akitoa maelezo kwa Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, Rosemary Senyamule (wa pili kushoto), alipotembelea kukagua soko hilo jana, ambalo limekamilika kwa asilimia 100. Kushoto ni Naibu Meya wa Jiji hilo, Jamal Ngalya na Mwakilishi wa Mkurugenzi wa Jiji, Upendo Rweyemamu. **PICHA: PETER MKWAVILA**

# Lishe kupunguza utoro wanafunzi

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

SERIKALI imewataka wadau wa lishe kushiriki na kusaidia mpango wa lishe shuleni ili kusaidia kupunguza utoro na kuongeza mahudhurio na umakini wa wanafunzi darasani.

Naibu Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Omary Kipanga, alibainisha hayo juzi kwenye hafla ya kutia saini fomu ya muungano wa lishe shuleni iliyotengenezwa na Shirika la Mpango wa Chakula Duniani (WFP) jijini hapa.

Kipanga alisema mradi huo ni muhimu sana kwa shule kutokana na kwamba unasaidia kuchochea mahudhurio ya wanafunzi, usikivu wa darasani lakini pia kuwajengea afya bora wanafunzi wanaohudhuria shuleni hapo.

"Naishukuru sana serikali kwa kukubali suala la uwepo wa lishe mashuleni kwa sababu kitu hicho kimezidi kupanua uwigo wa usikivu kwa wanafunzi kwa sababu wanakuwa wamepata chakula,"alisema Kipanga.

Alisema muungano huo Tanzania ni muhimu kwa sababu utawezesha wadau wa maendeleo kuendelea kuhamasisha umuhimu wa chakula shuleni.

Aliipongeza serikali kutokana na kukubaliana na suala la uwepo wa chakula shuleni kwa sababu unasaidia kwa kiasi kikubwa kuchochea mahudhurio shuleni. Aliwapongeza pia WFP kutokana na kuleta mradi huo mashuleni huku akisisitiza Shirika hilo limeona namna gani lishe ilivyo muhimu kwa wanafunzi.

Naye Mkurugenzi Mkazi wa WFP, Sarah Gordon-Gibson, alishukuru Serikali ya Tanzania kutokana na ushirikiano inaoonyesha katika kazi inazofanya nao katika masuala ya lishe.

Godon alisema mpango wa chakula mashuleni ni mzuri sana kwa sababu unasaidia watoto kuelewa masomo yao vizuri kitendo kinachochangia kuongeza ufaulu darasani. Mkurugenzi Mkazi huyo alisema WFP itaendelea kusisitiza nchi kujiunga katika mpango huo ambapo hadi sasa tayari nchi 52 zimeshasaini fomu hiyo.

Awali, akimkaribisha mgeni rasmi, Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, Riziki Mdoe, alisema suala la lishe shuleni ni la muhimu, hivyo WFP imefanya jambo la muhimu kwa kutia saini mkataba huo.

# Watakiwa kuchangamkia msamaha wa Rais wa kodi

**Na Peter Mkwavila,** DODOMA

MRATIBU wa Kodi Jiji la Dodoma, Matilda Mactavo, amewahimiza wakazi wa Jiji la Dodoma kuchangamkia fursa iliyotolewa na Rais Samia Suluhu Hassan ya msamaha kwa wanaodaiwa riba ya kodi ya pango la ardhi.

Hivi karibuni, Rais Samia alitangaza msamaha huo kwa wananchi kulipa kodi ya pango la ardhi kwa wanaodaiwa kuanzia Julai hadi Desemba, mwaka huu, bila kutozwa riba.

Mratibu huyo aliyasema hayo jana alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari kuhusu umuhimu wa kuitumia nafasi hiyo.

"Niwaombe wananchi wa Jiji la Dodoma kuitumia nafasi hii ambayo imetolewa na Rais kwa wale wanaodaiwa pango la ardhi walipe bila ya kutozwa riba,"alisema.

Kwa upande wake, Mkuu wa Idara ya Mipango Miji wa Jiji hilo, Joseph Nkuba, aliwahimiza wananchi wa Jiji la Dodoma kuchangamkia fursa hiyo ambayo Rais ameamua kuwapunguzia mzigo wa gharama ya deni la msingi lililosamehewa.

Nkuba alisema kuwa Halmashauri ya Jiji bado inaendelea kutoa elimu kwa wananchi juu ya ulipaji wa kodi zinazotakiwa kulipwa kupitia vitengo vyake.





# Bil. 36/- kunufaisha wakulima mwani

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

JUMLA ya Sh. bilioni 36 zimetolewa kwa wajasiriamali wanawake wenye nia ya kujikita katika kilimo cha mazao ya baharini kikiwemo cha mwani ambacho hulimwa na wanawake kwa asilimia 90.

Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango, Dk. Saada Mkuya Salum, alisema hayo jana wakati akitoa ufafanuzi kuhusu mikakati ya serikali ya Zanzibar kuwakomboa wanawake kuingia katika shughuli za ujasiriamali wa mazao ya baharini katika kikao cha Baraza la Wawakilishi.

Alisema kwa upande wa kilimo cha Mwani, Serikali ya Mapinduzi Zanzibar (SMZ) imefanya juhudi kubwa na imepanga kutengeneza boti 500 kwa wakulima wa Mwani ili kuwawezesha kufika katika eneo lenye kina kikubwa cha maji.

Dk. Mkuya alisema katika kuona wanawake wanapiga hatua kubwa katika kilimo cha mwani, serikali imeanza ujenzi wa kiwanda cha kusarifu na kuongeza thamani zao hilo katika eneo la Chamanangwe, mkoa wa Kaskazini Pemba.

"Tumeanza kujenga kiwanda cha kusarifu na kuongeza thamani ya mwani kwa wakulima ambapo matumaini yetu makubwa bei ya mwani itaongezeka na wakulima kupata kipato kinachostahili na kazi za kilimo hicho," alisema.

Aidha, alisema katika fedha hizo, wanawake wanatakiwa kujitokeza kujikita zaidi katika shughuli za ufugaji wa samaki, majongoo bahari na kaa kwa ajili ya kupata kipato kikubwa.

Waziri alisema ufugaji wa mazao ya baharini yakiwamo samaki na majongoo bahari ni miongoni mwa vipaumbele vya SMZ katika kuelekea uchumi wa bluu ili wananchi kujikomboa kiuchumi na uwekezaji.

"Tunawataka wanawake wajitokeze kwa wingi kuchangamkia fursa ya fedha za UVIKO - 19 ambazo zimetengwa kwa ajili ya uchumi wa bluu katika mazao ya baharini kuona walengwa ambao ni wanawake wanajikomboa kiuchumi na kupiga hatua kubwa ya maendeleo," alisema.



Naibu Waziri wa Maendeleo ya Ustawi wa Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Anna Athanas Paul, akizungumza katika kikao cha Baraza la Wawakilishi, Chukwani Zanzibar jana. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# Sheria ya mtoto kufanyiwa mapitio

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

SERIKALI ya Mapinduzi ya Zanzibar (SMZ) imesema inakusudia kuifanyia mapitio Sheria ya Mtoto Namba 6 ya mwaka 2011 ili kuleta mabadiliko makubwa ya kupambana na vitendo vya udhalilishaji wa kijinsia na kuwawezesha watoto kupata fursa na haki zote kwa mujibu wa sheria.

Hayo yalisemwa jana na Naibu Waziri wa Maendeleo ya Jamii,Jinsia Wazee na Watoto, Anna Athanas Paul, wakati akijibu swali la Mwakilishi wa Dimani, Mwanaasha Khamis Juma , aliyetaka kujua lini serikali itaifanyia marekebisho Sheria ya Mtoto ya mwaka 2011 ili kukabiliana na matukio ya udhalilishaji wa kijinsia kwa watoto kwa mujibu wa mikataba ya kimataifa.

Naibu Waziri huyo alisema sheria ya mtoto ni muhimu katika kulinda mikataba ya kimataifa ikiwemo wa haki za watoto (CRD) wa mwaka 1979.

Alisema kumejitokeza changamoto nyingi katika sheria ya mtoto ambayo imeibua matukio ya vitendo vya udhalilishaji wa kijinsia ambayo huwakosesha watoto haki zao za msingi.

Sheria ya sasa ya mtoto, alisema haijaweka adhabu ya makosa ya udhalilishaji kwa mtoto wa kike zinazohusiana na makosa hayo.

Alisema wizara inakusudia kufanya mapitio ya sheria hiyo kwa kuwashirikisha wadau mbalimbali wanaofanya kazi ya utetezi kwa wanawake na watoto ili kupata michango ya makundi yote.

Naibu Waziri huyo alisema wizara imejipanga kufanya mapitio ya nyumba salama ambazo zipo kwa ajili ya kuwahifadhi watoto wanaopata vitendo vya udhalilishaji wa kijinsia kwa ajili ya kuwaliwaza.

Aidha alisema wizara inakusudia kuweka kanuni na matunzo na kinga ya watoto pamoja na kanuni za kuweka watoto kwa wazazi walezi.

"Hayo ndiyo maeneo ambayo tumejipanga kuhakikisha tunakutana na wadau wenzetu katika kuifanyia mapitio sheria ya mtoto ili ifanye kazi vizuri na kupambana na matukio yote ya udhalilishaji wa kijinsia,' alisema.

# Wahimizwa kilimo cha mtama, kunde

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

WAKULIMA wisiwani Zanzibar wametakiwa kujikita zaidi kulima mtama, kunde na choroko ambayo yanao uwezo mkubwa wa kustahamili ukame na ukosefu wa mvua.

Hayo yalisemwa jana na Waziri wa Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo, Shamata Shaame Khamis, wakati akijibu swali la Mwakilishi wa Kojani, Hassan Hamad Omar.

Mwakilishi huyo alitaka kujua sababu za kutoweka kwa kilimo cha maweni ikiwamo mtama ambacho kina uwezo mkubwa wa kustahamili mazingira ya ukame.

Khamis alisema kilimo hicho kilikuwa maarufu katika maeneo ya Maweni ambako wakulima huzalisha mtama, kunde, choroko na mbaazi.

Hata hivyo alikiri kudorora kwa kilimo hicho kutokana na sababu mbalimbali ikiwamo mabadiliko ya tabia ya nchi pamoja na wananchi wengi kujikita katika kilimo cha mboga chenye kipato cha haraka.

Alisema wakulima wengi wakiwamo waliokuwa wakilima maeneo ya Maweni hivi sasa wamejiingiza katika kilimo cha mboga na matikiti maji ambacho matokeo yake yameonyesha kupata mafanikio makubwa.

"Mheshimiwa Spika niwaambie wajumbe wa Baraza la Wawakilishi kuwa kilimo cha maweni kimepungua sana. Wakulima wake wamejikita na kujiingiza katika kilimo cha mboga na matikiti maji ambacho kipato chake ni kikubwa," alisema.

Khamis aliwataka wakulima kuendelea kulima kilimo cha viungo ikiwemo Vanila na Pilipili manga ambacho kimeonesha kipato kikubwa na soko la uhakika nje ya nchi.

Waziri alizipongeza asasi za kiraia ikiwamo jumuiya za kimataifa ambazo zimekuwa zikitoa elimu na kuwapatia mbegu wakulima hao ili kulima kitaalamu zaidi na kupata tija ya mapato mazuri.

"Wizara ya Kilimo tumeanza kuwashajihisha wakulima wetu kuona wanalima kilimo cha mazao ya viungo ambapo soko lao lipokubwa la uhakika nje ya nchi hatua ambayo itawawezesha kupata kipato kikubwa," alisema.

Nipashe
MWANGA WA JAMII
BT
BURUDANI TELE
JUMAMOSI SEPTEMBA 17, 2022



KANYE ALITIBUA TENA

Ukurasa.12



# ukimya ni busara

NYOTA wa muziki wa Bongo Fleva, Omari Nyembo, maarufu kama Ommy Dimpoz, ameibua gumzo wiki hii baada ya kuibuka majibizano na baba yake mzazi.

Mvutano huo ulianza baada ya baba yake Mzee Faraji Nyembo, kueleza namna anavyohangaika kukidhi kipato chake kwa kuendesha bajaji katika mitaa ya mji wa Sumbawanga.

Kupitia mahojiano na redio moja, Mzee Nyembo alisema anamshukuru Mungu kutokana na chombo hicho kumuingizia pesa ambazo zinatosha kukimu maisha yake na familia kwa ujumla.

Hata hivyo, baadhi ya watu waliingilia kati na kumtaka Ommy Dimpoz, kukaa kimya kwani kuendeleza maneno ni kama wanawanufaisha watu.

Mgogoro wa kama huo umewakumba mastaa wengi nchini ambao walijikuta katika wakati mgumu kutokana na maoni kinzani kutoka kwa watu tofauti.

Diamond Platnum, alikuwa mmoja wa wasanii aliyekuwa na mvutano wa kushindwa kumtunza Mzee Abdul, kwa miaka mingi mpaka msanii alipoamua kuweka wazi kwamba huyo hakuwa baba yake mzazi ndipo ulipoisha.

Hata hivyo, kwa miaka mingi Diamond alionekana kunyamaza kimya, huku mzee Abdul akilalamika kwamba hapati matunzo kutoka kwa mwanamuziki huyo na badala yake mama yake mzazi ndiye anayethaminiwa.

Wachambuzi wa muziki wanasema kitendo cha Ommy Dimpoz, kumjibu baba yake mitandaoni haikuwa sahihi kwani alitakiwa kujifunza kwa wasanii wenzake ambao walipitia katika hali hiyo na kisha walifaulu kuyamaliza.

"Ommy Dimpoz alitakiwa kujifunza kwa Diamond na wengine waliopitia hali hiyo, kujibizana na wazazi katika mitandao sio jambo sahihi hata kama ana haki, alitakiwa kunyamaza kwani kufanya hivyo ni busara," amesema Japhet Kalima.

Amemshauri kutafuta ufumbuzi wa tatizo hilo kwani licha ya baba yake hakumtunza wakati alipokuwa mtoto, haiwezekani kulipiza kisasi.

BASI SAWA

## Kanye alitibua tena



RAPA na mfanyabiashara Kanye West 'YE' anaripotiwa kuwa amefikia maamuzi ya kuvunja mkataba wake na Kampuni Ya GAP iliyokuwa ikihusika na uuzaji pamoja na usambazaji wa bidhaa zake.

Kwa mujibu wa ripoti iliyotolewa na mtandao wa Wall Street Journal, Kanye West ameamua kumtuma mwanasheria wake Nicholas Gravante Jr, kuitaarifu GAP kuwa anasitisha mkataba wa ubia katika usambazaji na uuzaji wa bidhaa zake, ikiwa ni miaka bado imesalia minane mkataba kumalizika.

Fahamu, mkataba wa YE na GAP ulianza rasmi mwaka 2020, ambapo alisaini kusimamiwa kwa miaka 10 na kampuni hiyo.


## Zabron Singers wamshukuru Mungu

WAIMBAJI wa kundi la Zabron Singers, wamesema imekuwa kama zawadi kutoka kwa Mungu baada ya kualikwa kutumbuiza katika sherehe ya kuapishwa kwa rais mpya wa Kenya.

Kiongozi wa Zabron Singers, Japhet Zabron amesema wanashukuru jinsi raia na kiongozi mpya wa nchi hiyo Willium Ruto, kuwapokea na kufurahia nyimbo zao pale walipoimba uwanjani.

"Imekuwa kama bahati na zawadi ya Mungu imetufikia kwani tukio la kutumbuiza mbele ya viongozi wa mataifa mbalimbali na wanachi sio la kawaida kwetu. Tulijiamini tangu tulipopewa mwaliko na tulipoingia kuimba kila kitu kilikuwa sawa," amesema Japhet.





## Harmonize, Kajala hayupo wa kuwasumbua

MAMBO yanazidi kuiva kwa mastaa Harmonize na Kajala masanja, kiasi ambacho wawili hao wameapa iwe jua au mvua hawawezi kutengana tena.

Akizungumza hivi karibuni Kajala amesema, kosa walilofanya kipindi cha nyuma haliwezi kujirudia na kwamba kwa sasa anajihisi kama malaika kutokana na mapenzi anayopata.

Mwaka mmoja uliopita wawili hao waliachana kutokana na tuhuma ya Harmonize kumtaka kimapenzi paula ambaye ni mtoto wa kajala, lakini mwenyewe alikanusha vikali.



## Dulisykes aomba aachwe

MKONGWE katika muziki wa Bongo Fleva, Prince Dullysykes, amesema havunjiki moyo kutokana na tuhuma anazopata kutoka kwa wasanii wenzake wa muda mrefu kuwa anapenda kushirikiana na waimbaji wachanga.

Amedai, wasanii wenzake wakongwe wanamuona mjinga kuona anafanya kazi na wasanii wa wapya katika tasnia ya muziki wa Bongo Fleva.

"Kila ninachokifanya naamini nipo sahihi, wapo wanaoniona mimi ni mjinga kushirikiana na wanamuziki wa sasa, lakini kwangu hilo halinisumbui," amesema Dullysykes.

## Mapigo ma 5 Sikinde

**Na Adam Fungamwango**

MWIMBAJI wa bendi ya DDC Mlimani Park Orchestra, Abdallah Hemba ametangaza rasmi kuliacha kundi hilo na kukaribisha makundi mengine ambayo yanamuhitaji.

Hata hivyo, kuna taarifa kuwa kuna kundi lingine liitwalo Sikinde Original ambalo limeanzishwa na ndilo lililosababisha kuwapo na sintofahamu kwenye bendi hiyo.

Ingawa hakusema kama yupo kwenye bendi hiyo, lakini Hemba alisema kama kundi hilo litamhitaji, basi yeye hana matatizo.

Habari zinasema si Hemba tu, bali kuna wimbi la wanamuziki sita kulihama kundi hilo, kutokana na kutokea sintofahamu kati yao na uongozi.

Kiongozi wa bendi hiyo, Habib Jeff, alisema tatizo kuwa na nidhamu na kwamba kilichotokea, Hemba na wenzake watano walichelewa ukumbini na mkuu wa nidhamu Hassan Kunyata, aliwasimamisha kwa muda wa siku moja, kitu ambacho kimesababisha yote haya.

Tayari, Sikinde wamechukua hatua za kuanza kuziba mapengo kwa kumchukua mwimbaji wa zamani wa kundi hilo, Hussein Jumbe, na mpiga rhythm wa zamani wa bendi za Mwenge Jazz na Vijana Jazz, Shomari Ally kuziba mapengo.

Hii si mara ya kwanza kwa Sikinde kuondokewa na lundo la muziki, kwani imeshatokea huko nyuma na kupata mapigo kadhaa.

### Mulenga na wenzake walivyotimka

Mpiga solo Joseph Mulenga, Abdallah Gama mpiga rhythm, na mpiga bass, Selemani Mwanyiro waliondoka kwenye kundi hilo mwaka 1984 na kuwa pigo la kwanza wa Sikinde.

Ilikuwa waondoke na mwimbaji Hassan Rehani, Bitchuka, lakini alikuwa likizo kwao Kigoma, hivyo alichelewa kurudi na nafasi yake akachukuliwa Shaaban Dede.

### Gurumo na Bitchuka walivyotoka

Mwaka 1985, kiongozi wa bendi hiyo Muhidini Maalim Gurumo na Bitchuka, pamoja na wanamuziki wengine alilipa kisogo kundi hilo na kwenda Orchestra Safari Sound lililokuwa limeondokewa na kiongozi wake Freddie Ndala Kasheba, aliyekuwa anatumia mtindo wa 'dukuduku'.

Gurumo na wenzake wakaanzisha mtindo wa 'Ndekule'. Hilo lilikuwa ni pigo la pili kubwa kwa Sikinde.

### Chidumule na Bushoke wakafuata

Sikinde ambayo ilibaki na Coasmas Chidumule na Max Bushoke kama waimbaji wakuu, ilipata pigo la tatu, baada ya wanamuziki hao nao kuchukuliwa na Ndekule mwaka 1986.

Hii ni baada ya Bitchuka kurejea Sikinde, ambapo nao wakaamua kuacha na kwenda kule alikotoka.

### Gurumo alivyomzoa tena Bitchuka

Baada ya kupata vyombo vipya mwaka 1990, ikitaka kuboresha kundi, bendi ya Juwata Jazz 'Msondo Ngoma', ilimtaka Gurumo na Bitchuka. Ilikuwa rahisi kumpata Gurumo, lakini si Bitchuka ambaye alikuwa Sikinde.

Kilichofanyika, Guruma alijifanya anarejea Sikinde, lakini nia yake ni kwenda 'kumzoa' Bitchuka, siku chache wote watatangazwa kuwa ni wanamuziki wa Msondo.

### Jumbe alivyoitosa Sikinde

Miezi michache kabla ya TX Moshi William, kufariki mwaka 2006, alipendekeza achukuliwe Hussein Jumbe, achomolewe Sikinde na kuletwa Msondo, lililokuwa moja ya pigo lingine kwa bendi hiyo.



GURUMO



## Sirudi Kijijini, Baba mzima ovyo!

**Na Adam Fungamwango**

MWANAMUZIKI Remmy Ongala, wakati wa uhai wake alishawahi kuimba wimbo mmoja ambao unaitwa 'Hanifa'. Maudhui ya wimbo huo ni kwamba baba mwenye nyumba anamfuata mke wa mpangaji wake na kuanza kumuuliza maswali. Lakini alikuwa na lake jambo.

Alimuuliza jina, anatoka wapi, na mwishoni akamwambia watoto wazuri kama yeye wakija mjini wanatakiwa wawaone watu kama yeye wapate kila kitu bure na siyo kujipachika kwa wanaume waokota makopo gerezani kama mume wake.

Labda kutokana na lugha ya kuzunguka aliyoitumia, mwanamke hakuelewa somo. Akamwambia basi ngoja asubiri mume wake akija atamueleza kuwa wamepewa chumba cha bure. Matokeo yake baba mwenye nyumba akakasirika na kumwambia akija mumewe wafungashe na wahame.

Nia kubwa mzee yule alikuwa anamtaka yule dada. Jambo hili lipo sana kwenye jamii yetu hata leo.

Hata filamu hii iitwayo 'Sirudi Kijijini' haipo mbali sana na hilo.

Imechezwa na Yahaya Maulidi aliyecheza kama Msonga, Ally Omari kama mzee Tosha, Rehema Alfred, yeye alicheza kama Ray, Fadhila Salum, akicheza kama Salha, Juma Omari kama Vobo na wengineo.

Msonga na rafiki yake Magenge wakatoka kijijini na kulivamia jiji la Dar es Salaam, ambalo lina raha na karaha.

Stori zao walizokuwa wakipiga vijiweni huko kijijini kuhusu maisha ya Dar, sivyo walivyoyakuta.

Hakuna maisha mazuri, wala watu hawalali kwenye maghorofa, pia si watu wote wana maisha mazuri.

Mjini ukiwa na kazi, biashara au shughuli halali hakuna shida, lakini kama unabangaiza ni matatizo.

Wanafika Dar na kuhangaika, hawana la kula wala kulala. Wanaishi maisha ya tabu ya kulala stendi na kwenye baraza ya nyumba za watu.

Walibangaiza sana wakapata pesa ambazo waliamua kutafuta chumba ili wapange. Lakini kila wanapokwenda wanaambiwa hawapangishi watu ambao hawajaoa.

Jambo hili linawakwaza sana kiasi kwamba wanakaa na kutafakari nini wafanye. Wazo linawajia kuwa mmoja kati yao ajifanye kuwa ni mke ili waweze kukubaliwa, ingawa ukweli wenyewe wanaujua.

Msonga ndiye aliyejifanya mwanamke, akajifunika khanga na wakaenda kuomba chumba kwa mzee Tosha, wakakubaliwa.

Magenge sasa kazi yake ni kwenda kubangaiza ili kupata pesa ya kula, Msonga anabaki ndani akijifanya mwanamke. Hakutakiwa kutembeatembea kwani itajulikana na watafukuzwa. Lengo ni mpaka wapate pesa ya kodi ambayo itawafanya waweze kwenda kupanga nyumba zenye hadhi ambazo zenyewe hazina masharti maarufu kama 'apatimenti'.

Mzee Tosha, akadhani ni kweli mpangaji wake yule ni mwanamke, hivyo akitoka msalani amsalimia na kumtongoza.



# R Kelly bado aandamwa

NYOTA wa R&B Robert Kelly maarufu kama R. Kelly (55) amepatikana na hatia ya unyanyasaji wa kingono wa watoto katika kesi ya pili iliyoendeshwa na mahakama ya shirikisho.

Jopo la mahakama lilimpata na hatia ya makosa sita kati ya 13 katika kesi ya wiki nne iliyoendeshwa katika mji wa wa Chicago.

Mwaka jana muimbaji huyo wa Bump n' Grind alipatikana na hatia ya usafirishaji haramu wa watu kwa ajili ya ngono na wizi wa ulaghai na kuhukumiwa kifungo cha miaka 30 jela.



## Nyota Ice Prince sasa huru

STAA wa muziki wa Hip hop, wa Nigeria Ice Prince, hatimaye ameachiwa huru baada ya kuwa ndani kwa wiki kadhaa.

Kulingana na wakili wake Folarin Dalmeida, msanii huyo ameachiliwa huru mwanzoni mwa wiki baada ya kukamilisha masharti ya dhamana.

"Masharti ya dhamana yake yametimizwa, na aliachiliwa jana," alisema.

Itakumbukwa kuwa wakati wa kesi hiyo Jumatano, wakili wa upande wa mashtaka aliomba mahakama kuahirisha kesi hiyo, akitaja kutokuwapo kwa mashahidi wake wawili.

## Wengi wamlilia PnB Rock

RAPA wa Marekani, Rakim Hasheem maarufu kama PnB Rock, ameuawa kufuatia tukio la wizi wa kutumia silaha katika jiji la Los Angeles.


PnB Rock, ambaye alizaliwa mwaka 1991 ameacha mtoto mmoja.

Kulingana na Idara ya Polisi ya Los Angeles, Kapteni Kelly Muniz, wakati wa mkutano wa waandishi wa habari, majambazi hao walivamia mgahawa na kumtaka marehemu kuwapa fedha.

"Wakati wa tukio hilo, angalau mshukiwa mmoja alimwendea mwathiriwa na shahidi wa kike ndani ya mgahawa huo walipokuwa wakila na kudai watoe mali," alisema.

Baada ya majibizano ya maneno, mshukiwa alimpiga risasi mwanamuziki huyo mara nyingi na kisha kutoroka kwa kutumia gari.





## Steflon hujui mpenzi wa zamani haachwi?

RAPA wa kike wa Uingereza, Steflon Don, ameujibu wimbo wa aliyekuwa mpenzi wake Burna Boy unaoitwa 'Last Last' ambao wengi wanaamini ulihusu uhusiano wao.

Katika mazungumzo ya hivi majuzi na TT Torrez, nyota huyo wa muziki aliulizwa jinsi uhusiano wake na mwimbaji huyo ulivyoharibika

Alipoulizwa kama alifikiri Burna Boy alimuimba katika wimbo huo, Steflon Don alisema baadhi ya sehemu ya mashairi yalikuwa ya uongo.

"Yeye alikuwa na kitu ndani yake kuhusu mimi ni kama uwongo." Amesema.

## Baba Ijesha alilia kuliona jua

MUIGIZAJI wa Nollywood, Olanrewaju James, maarufu kama Baba Ijesha, ameiomba Mahakama ya Ukatili wa Nyumbani na Jinsia ya Ikeja kumpa dhamana wakati akisubiri hatma ya rufaa yake.

Msanii huyo ambaye amehukumiwa kifungo cha miaka mitano kutokana na ubakaji na unajisi wa watoto, amekata rufaa katika mahakama kuu ya Lagos, kupinga hukumu hiyo.

Baba Ijesha, anajaribu kutafuta njia ya kutoka gerezani na kuiomba mahakama hiyo kumpatia dhamana katika kipindi chote wakati mahakama kuu inapitia hukumu hiyo.






Baadhi ya wanafunzi wakiwa na mabango yenye ujumbe unaohamasisha vita dhidi ya rushwa hiyo. **PICHA ZOTE: SABATO KASIKA**

# Rushwa ya ngono shuleni inavyopingwa kila kona

## ■WAJIKI wapita kata kwa kata

**Sabato Kasika**

RUSHWA ya ngono ni moja ya vikwazo vinavyowakabili wanafunzi wa kike wanaosoma shule za msingi, sekondari na vyuo, na kusababisha baadhi yao kushindwa kufikia malengo.

Baadhi ya walimu na wahadhiri wamekuwa wakitajwa kujihusisha na rushwa hiyo, kwa kuwataka kimapenzi wanafunzi ili wawasaidie katika masomo au mitihani.

Wakati wanafunzi wakikabiliana na hali hiyo katika maeneo ya kutolea elimu, wanakumbana na vikwazo kama hivyo katika vyombo vya usafiri kama bodaboda, bajaji na daladala.

Mazingira hayo ya rushwa, yamelifanya Shirika la Wanawake Katika Jitihada za Kimaendeleo (WAJIKI), la jijini Dar es Salaam, kuendesha kampeni ya kukomesha rushwa ya ngono katika wilaya tatu.

Wilaya hizo ni za Kinondoni, Ilala na Temeke ambako inatolewa elimu ya madhara ya rushwa ya ngono ili kuhakikisha wanafunzi wanasoma bila vikwazo.

Hivi karubuni, WAJIKI ilizindua awamu ya tano ya kampeni inayofahamika 'safari salama bila rushwa ya ngono kwa wasichana inawezekana', ambayo inatarajiwa katika wilaya hizo kwa kipindi cha miaka miwili.

Mkurugenzi Mtendaji wa WAJIKI, Janeth Mawinza, anasema shirika limepata ufadhili kutoka Women Fund Tanzania (WFT), wa Sh. milioni 80, kwa ajili ya kampeni hiyo mwaka 2022/23, ili kunusuru wanafunzi dhidi ya kikwazo hicho.

Anasema wamepanga kufikia kata 18, kwa maana ya kwamba kila wilaya watafika katika kata sita kuendeleza mapambano dhidi ya rushwa ya ngono, ili kuhakikisha wanajenga uelewa mpana wa jamii juu ya masuala ya rushwa ya ngono na athari zake kwa watoto hasa wa kike.

"Tulizindua awamu ya tano ya kampeni hii wiki iliyopita, sasa tunaendelea kutembelea shule na kukusanya wanafunzi na kuzungumza nao, vijiwe vya bodaboda, daladala, bajaji na hata kugawa vipeperushi," anasema Mawinza.

Anafafanua kuwa wanafunzi wanaelimishwa kujua viashiria vya rushwa hiyo ikiwamo kupewa lifti, zawadi mbalimbali ambazo mwisho wake hujikuta wakiingia kwenye mtego bila kujua.

"WAJIKI inataka kujenga sauti na uwezo wa pamoja, ili wanaume washiriki katika utetezi na uchechemuzi wa haki za wanawake, hasa ukatili wa kijinsia na rushwa ya ngono na kukuza mtandao utakaoendesha kampeni inayobeba nguvu za pamoja kulinda na kutetea haki za kundi hilo," anasema.

Mawinza anasema lengo ni kutaka kuwa na Tanzania isiyo na ukatili wa kijinsia na yenye maisha bora.

Anaeleza kwamba wamedhamiria kutumia mbinu shirikishi ili kukuza uelewa wa haki za binadamu na ukatili wa kijinsia na kupunguza umaskini uliokithiri kwenye jamii.

"Tangu tuanze kampeni hii mwaka 2018, wadau wa vyombo vya usafiri na wengine wanaokataa rushwa ya ngono kwa wanafunzi na vitendo vingine vya unyanyasaji wa kijinsia," anasema.

Anawataja wadau wengine hao kuwa ni madereva teksii,mabasi makubwa, makondakta na viongozi wa serikali za mitaa, halmashauri za wilaya na taasisi zingine.

Aidha, Mawinza anasema awamu ya kwanza hadi ya nne ya kampeni hiyo, wameafiki madereva 3,742 na wanafunzi wa shule 24.

Kiongozi wa madereva wa bodaboda eneo la Makumbusho, Godvoice Kayombo, anasema umefika wakati sasa nao wapangiwe vipindi maalumu darasani ili watoe elimu kuhusu rushwa hiyo kwa wanafunzi.

Kayombo anasema vipindi vya dini vingetumika pia kuelimisha wanafunzi kuhusu athari za rushwa ya ngono.

"Tumekuwa tukitoa elimu kwa kukusanya wanafunzi eneo moja shuleni, lakini ninadhani ipo haja sasa ya kuambatana na walimu wa dini, ili tugawane zile dakika nasi tupate nafasi kuzungumza na wanafunzi,"anasema.

Anafafanua kuwa katika vipindi vya dini kuna utulivu wa kutosha na kwamba wanafunzi wanaweza kusikiliza vizuri zaidi kuliko kukusanya pamoja kwenye uwanja na kuwaelimisha.

"Siyo kwamba ninapinga utaratibu unaotumika sasa, ila lengo langu ni kutaka kuboresha kampeni hii ambayo tunaifanya kwenye vijiwe vya madereva wenzetu ambao hawajabadili mtazamo wao kuhusu rushwa ya ngono," anasema.

Mwalimu Mkuu wa Shule ya Msingi Minazini, Mwanyamala jijini Dar es Salaam, Esther Chambo anasema kampeni hiyo ikiwa endelevu, inaweza kusaidia wanafunzi wengi kuwa makini dhidi ya rushwa ya ngono.

"Ni kweli watoto wetu wanarubuniwa kwa lifti za bodaboda, hali ambayo inaweza kuwaingiza katika rushwa ya ngono na kujikuta wakikwama kuendelea na masomo, tuungane kupiga vita rushwa hii," anasema Chambo.

Anasema WAJIKI imesaidia shuleni kwake kwa wanafunzi kutambua viashiria vya rushwa, ikiwamo kupewa lifti au zawadi.

Mkuu wa Dawati la Elimu kwa Umma wa TAKUKURU Mkoa wa Kinondoni, Bibie Msumi, yeye anawataka wanafunzi, wanawake na jamii kwa ujumla kutofumbia macho rushwa ya aina yoyote.

"Taarifa ya rushwa itolewe kuanzia ngazi ya familia, na kama haifanyiwi kazi, mhusika asonge mbele na ikiwezekana afikishe taarifa ofisini kwangu kama ataona huko alikoanzia anazungushwa,"anasema.

Ofisa Ufuatiliaji na Tathmini wa WAJIKI, Hans Obote, anasema tangu kampeni hiyo ianze, imesaidia kuongezeka kwa taarifa za ukatili zilizo ripotiwa na uchukuliwaji wa hatua kwa dhati kwa jamii.

"Kumekuwapo na mipango au mikakati thabiti na endelevu ya kuzuia na kushughulikia matukio ya ukatili wa kijinsia, hivyo tunaamini kuwa awamu hii ya tano itazidi kuongeza uelewa wa kuhusu rushwa hiyo," anasema Obote.

Obote anasema wameimarisha uendeshaji wa klabu mbalimbali za kampeni ya kupinga vitendo vya rushwa kwa wanafunzi, wanawake na watoto wa mitaani.

"Tumewatambua na kuwajengea uwezo madereva wa daladala, bajaji, bodaboda, na Teksi na vikundi vya wanawake ili waweze kuitekeleza kampeni," anasema.



Mwalimu mkuu wa Shule ya Msingi Minazini, Esther akishiriki kampeni ya kutoa elimu kuhusu madhara ya rushwa ya ngono ilioendeshwa na WAJIKI shuleni hapo wiki iliyopita.

TULIKOTOKA, TULIPO & TUNAKOKWENDA...



Na Adam Fungamwango

# Wimbi la vijana kuzamia meli lilivyotikisa

## ■Mabaharia walizuzua akili wengi
## ■Masela' wakashinda feri, 'docks'



BENDI ya muziki wa dansi ya Vijana Jazz mwishoni mwa miaka ya 1980, walitunga wimbo mmoja, mtunzi wake ni Adam Bakari, uitwao 'Ngapulila'.

Wimbo huu ulielezea juu ya kijana mmoja Ngapulila kuwa na mawazo ya kutaka kuzamia meli ili aende ng'ambo kutafuta maisha kwani ya hapa nchini yalimshinda.

Akadai kuwa, anakula na kulala kwa tabu. Yeye aliamini kuwa akizamia na kufika barani Ulaya maisha yake yatakuwa mazuri.

Kwenye wimbo huo huo, rafiki yake anamsihi asifanye hivyo, badala yake afanye kazi kwa bidii hapa hapa nchini anaweza kufanikiwa kwani maisha ya kuzamia meli yana hatari kwa sababu anaweza kutoswa baharini na kupoteza maisha yake.

Wimbo huu unaelezea hali halisi ya miaka ya 1970 mwishoni mwa miaka ya 1980 kulipokuwa na wimbi kubwa la vijana wa Kitanzania kuzamia meli.

Vijana wengi wa Kibongo hasa kwenye Ukanda wa Pwani, Dar es Salaam, Pwani, Zanzibar na Tanga walikuwa vinara wa wa kuzamia meli.

Na hilo lilichagizwa sana na wale wazamiaji wa mwanzo kufanikiwa. Nadhani wakati ambao hakukuwa na wimbi kubwa la wazamiaji, waliofanya hivyo mwanzo na kukakamatwa walipewa kazi melini na kuwa mabaharia, hivyo waliporejea nchini, hali yao ya kimaisha ya wakati huo ilionekana ni nzuri sana.

Walirejea wakiwa na nguo ambazo ni tofauti na zilizokuwapo nchini. Walivaa majinzi, na nguo za thamani ambazo zilibabaisha vijana wengi sana.

Pesa walizozipata walizifanyia matanuzi ya nguvu kwenye mabaa na maeneo mengine ya starehe, na wale ambao waliojiongeza walijenga majumba.

Hawa walijiita 'sailor', yaani mabaharia, au wanamaji. Walikuwa na mbwembwe sana. Watoto wa mjini wakawaita 'masela'. Na ndiyo asili ya jina hilo ambalo kwa sasa wanajiita watoto wa vijiweni.

Hii iliwasukuma vijana wengi kuona kuwa kazi ya maana ili ufanikiwe kwenye maisha ni kuzamia meli.

Kumbuka wakati huo nchi haikuwa na nguo hizi za mitumba kama zilivyo sasa, hivyo nguo hizi zilivaliwa na mabaharia tu, tambo zao na matanuzi yaliwapa ukichaa vijana wengi ambao sasa wakawa hawataki kazi yoyote, bali kwenda Ulaya kutafuta maisha ili nao wawe na maisha mazuri, wenyewe wakati huo waliita 'kuukata.'

Na njia rahisi ni kuzamia meli. Walichokuwa wanafanya ni kusubiri meli ambayo inakaribia kuondoka. Ujanja na utoto wa mjini huwafanya kuingia ndani ya meli bila kujulikana na kwenda kujificha sehemu ambazo si rahisi kuonekana kwa wakati huo mara moja, labda baada ya msako mkali. Meli inapoondoka na baada ya wiki kadhaa wanajitokeza, ilikuwa imefika mbali sana. Huko watakamatwa na kuulizwa maswali, lakini baadaye wanapewa kazi humo humo na hapo wanakuwa tayari 'wameukata'.

Wakati mwingine wanashushwa kwenye nchi nyingine barani Ulaya ambako wanatokomea kusikojulikana, na kubanganiza kupata kazi yoyote ile ambayo itamfanya aishi.

Hata hivyo, ongezeko la vijana wengi kuambizana mchezo huo wakidhani watapata kazi, ulisababisha kadri miaka ilivyozidi kwenda kuanza kutendewa mambo mabaya, ikiwemo kutoswa kwenye maji, wakiwa katikati ya bahari.

Vijana wengi wa Kitanzania walipoteza maisha kwa sababu hiyo. Wakaja wenyewe kung'amua kuwa kuna aina fulani za meli ndizo zinafaa kuzamia na zingine hata kama wataacha milango wazi hakuthubutu, kwani walijua ni mdomo wa mauti.

Vijana wengi wakati huo walishinda feri, na bandarini wakati huo maarufu kama 'docks', ili kuangalia meli gani itakuja ili wazamie.

Kuna makosa ya kiufundi wakati mwingine waliyafanya kwa kuzamia meli na kwenda kujificha. Kumbe meli haiondoki kwa siku za karibuni. Matokeo yake wakiibuka wanakuta ipo pale pale, wakati wao wanadhani iko maili nyingi kutoka Bongo.

Kuna kisa kimoja kilidai kuwa jamaa alizamia, na baada ya muda akaibuka akidhani yupo karibuni kufika Ulaya, kumbe meli bado ipo Kigamboni.

Hii ilitokana na kwamba kuna wakati meli inaweza kutoka bandarini na kwenda mbele kupita feri, ikasimama mbali kwenye kina kirefu cha maji kule kwa siku kadhaa kupisha meli zingine zipakue mizigo. Yeye akadhani ilikuwa imeshaondoka.

Misemo yao ilikuwa ni 'one day yes', sea never dry'. Wakiwa na maana 'ipo siku' na 'bahari haikauki'. Yalikuwa ni maneno ya kufarijiana kuwa ipo siku moja na wao 'watauakata' kwa sababu bahari ipo na itakuwepo milele, kwa hiyo kuna siku tu watazamia ili kwenda kupata maisha mazuri ughaibuni, au ndani ya meli.

Kwa sasa mambo hayo hayapo tena kwa sababu mbalimbali hasa ya kimazingira na kiteknolojia.

Tanzania kwa sasa imeendelea sana, vitu vingi ambayo zamani vilikuwa vikiletwa na watu toka Ulaya kwa sasa vipo tu hapa, zikiwemo nguo, samani na vingi vinavyofanana na hivyo.

Pia, kuna fursa nyingi tu kama mtu atafanya kazi kwa bidii, biashara na kujishughulisha kwa namna yoyote ile.

Hebu tuangalie wadau wanasema nini, kwani kila mtu amejaribu kuielezea kwenye simu na mitandao ya kijamii, nilipoiweka mada hii.

"Bora wapambane hapa hapa tu. Wengi wakifika huko wanaishi kama swala anayewindwa, wanaishi kwa kujificha kuogopa kukamatwa. Matokeo yake hupoteza miaka mingi sana katika kubangaiza." Anasema mdau mmoja, mwingine ambaye yeye alishawahi kuzamia akaandika.

"Nakubaliana na wewe kabisa enzi za kupanda meli miaka ya 1980, na 1990 iliendana na ujasiri na uthubutu. Mimi ni miongoni mwa vijana wa mwanzoni kupanda meli na nilipanda meli Dar es Salaam, nilitembea nayo miezi sita, dah ni hatari sana. Kila zama na kitabu chake, enzi za kuzamia meli zilishapita, siku hizi watu wanaenda kwa ndege na kwa njia halali, maisha hayawezi kubaki na kuwa yale yale milele." Wadau hawa ambao kama kawaida huwa hawapendi majina yao yachapishwe, mmoja naye akasema.

"Zamani, miaka ya 1990 kurudi nyuma kuzamia kulikuwa kunaambatana na kufahamu lugha kama ya kiingereza ambayo ilisaidia kuelezea shida yako kwa nahodha.

Nahodha akiingiwa huruma na hapo mnazungumza mkiwa mbali na nchi uliyotoka anaweza kabisa kukusaidia kwa kukupa kazi za kusafisha humo ndani ya meli."

"Zamani kwanza ilikuwa bonge la sifa mtaani ukiitwa mpanda meli na mzamiaji hata ukikamatwa, hivi leo dunia ina matatizo mengi, kuna changamoto za ugaidi, uharamia wa wateka meli kushamiri ni hatari sana kupanda kuzamia, umejificha ndani ya bomba halafu unaibuka, unaweza ukala shaba," alisema mchangiaji mwingine.

"Wengine haikuwa lazima kwenda Ulaya, hata Sauzi tu, ikitua bandari za Beira, Maputo, Durban na Cape Town, watu wanatoka na kuingia mtaani," jamaa mwingine aliandika.

Mmoja akaandika hivi "Kuna meli zingine wazamiaji wakijua zinatoka nchi gani hawapandi hata waache mlango wazi, jaama walikuwa na roho mbaya sana, wanakutoka tu baharini."

Huyu wa mwisho akapigilia msumari akionyesha pia moja ya sababu ambayo sasa vijana hawazamii

"Nimepiga deiwaka sana pale bandarini, kwa sasa kuzamia ni ndoto, meli nyingi kwa sasa zimefungwa kamera za CCTV kwa hiyo ni rahisi sana kuonekana."

**Tuma meseji 0716 350434**

## HABARI KIMATAIFA

# Maelfu waendelea kumuaga Malkia, Ujumbe wa China wapigwa marufuku

**LONDON, Uingereza**

MAELFU ya waombolezaji wameendelea kujitokeza kuuaga mwili wa Malkia Elizabeth II ukiwa umelazwa katika Ukumbi wa Westminster jijini London.

Kufikia jana saa 7:00 mchana foleni ilikadiriwa kuwa na urefu wa maili 4.9 sawa na kilomita 7.8.

Watu wameonywa kwamba watahitaji kusimama kwa saa nyingi na fursa chache za kuketi chini, kwa kuwa foleni inasonga kila wakati.

Wale wanaojiunga na foleni wanapewa alama mikononi ili waweze kuondoka kuchukua kinywaji au kwenda msalani ikiwa wanahitaji.

Wakati huo huo, ujumbe wa serikali ya China umepigwa marufuku kuhudhuria katika jumba ambalo Malkia Elizabeth II atakuwa anaagwa.

Kulingana na BBC, Spika wa Baraza la Commons Sir Lindsay Hoyle. alikataa ombi la ujumbe huo kuingia katika kasri la Westminster kutokana na vikwazo vya China dhidi ya wabunge watano na wenzao wawili.

Malkia Elizabeth, ataagwa katika majengo ya bunge hadi mazishi yake siku ya Jumatatu.

Ofisi ya Spika iliiambia BBC kuwa haikuzungumzia masuala ya usalama.

Msemaji wa wizara ya mambo ya nje ya China alisema hawajaona ripoti kuhusu marufuku hiyo, ambayo iliibuka mara ya kwanza kwenye tovuti ya mwanasiasa.

''Kama mwenyeji, Uingereza kwa hakika inafahamu itifaki za kidiplomasia na tabia zinazofaa za kupokea wageni,'' alisema msemaji wa wizara ya mambo ya nje ya China, Mao Ning.

Mwaka jana, China iliweka marufuku ya kusafiri na kutaifisha mali kwa Waingereza tisa ikiwa ni pamoja na wabunge saba kwa kuishutumu nchi hiyo kwa kuwatendea vibaya Waislamu wa Uighur.

Hilo lilisababisha balozi wa China nchini Uingereza kupigwa marufuku kutoka Bungeni hatua ambayo sasa imechukuliwa hadi kwa ujumbe ambao ulitaka kutoa heshima zao katika jumba ambalo Malkia Elizabeth anaagwa.

Uhusiano wa Uingereza na China tayari umedorora na marufuku hiyo haiwezi kusaidia.

Hata hivyo, makamu wa rais wa China anatarajiwa kuhudhuria mazishi ya kitaifa itakayofanyika Jumatatu kando ya barabara kutoka jingo la bunge la Westminster Abbey.

Kulingana na kitabu cha sheria cha bunge Erskine May, mwaka 1965, Malkia Elizabeth II alikubali udhibiti wa kasri la Westminster ungegawanywa kati ya Lord Great Chamberlain ambaye ameteuliwa na mfalme na spika wa mabunge yote mawili.

**BBC**

# Eritrea yaamuru askari wa akiba kurudi jeshini

**ASMARA, Eritrea**

SERIKALI ya Eritrea inaendelea na zoezi la kuwakusanya wanajeshi wa akiba kwenda kwenye mapigano nchini Ethiopia.

Taarifa zilisema siku ya Alhamisi katika mji mkuu wa Asmara, idadi kubwa ya watu walipewa notisi na kupelekwa mstari wa mbele wa vita kwenye mpaka wa pamoja wa nchi hiyo katika eneo la Tigray.

Chanzo kimoja kiliiambia BBC kuwa askari wa akiba katika maeneo mengine mengi ya nchi hiyo pia wameambiwa kuripoti katika ofisi kuu.

Hivi karibuni shughuli za kuwasaka watu kurejea jeshini zimeimarishwa katika maeneo mengi ikiwa ni pamoja na Asmara.

Vikosi vya usalama vinawazuia watu kuangalia kama wana msamaha wa kutohudumu katika jeshi .

Baadhi ya askari wa akiba waliambiwa walete vifaa vyao wenyewe kama vile blanketi na chupa za maji, vyanzo vinasema.

Kulikuwa na matukio ya kina mama, watoto na wake wakilia wakati wa kuwaaga baba, kaka na waume zao.

Uhamasishaji wa hivi punde umezua hofu kwamba mzozo katika eneo jirani la Tigray nchini Ethiopia huenda ukaongezeka zaidi.

Mapigano kati ya serikali ya Ethiopia na vikosi vya Tigray yalianza tena mwezi uliopita baada ya kipindi cha mapigano kusitishwa.

Viongozi wa Tigray wameishutumu Eritrea kwa kuungana na kuwasiliana na Ethiopia katika maeneo ya magharibi ya mpaka wao wa pamoja.

Mamlaka zote za Ethiopia na Eritrea hazijajibu tuhuma hizo, lakini mamlaka ya Eritrea ilishutumu vikosi vya Tigray kwa kupanga kuwashambulia.

Vikosi vya Eritrea vilipigana pamoja na jeshi la serikali ya Ethiopia dhidi ya vikosi vya Tigraya katika awamu ya kwanza ya vita. Walishutumiwa kwa ukatili, lakini maofisa wa Eritrea walikanusha.

Marekani imeweka vikwazo kwa Wanajeshi wa Ulinzi wa Eritrea na chama tawala cha PFDJ kushiriki kwao katika mzozo wa Ethiopia.

**BBC**



Baadhi ya wakazi wa mji wa Izyum nchini Ukraine, wakirudi katika makazi yao baada ya eneo hilo kukombolewa kutoka vikosi vya Russia juzi. **PICHA: EPA**

# Ukraine yagundua kaburi la halaiki Izyum

**KYIV, Ukraine**

UKRAINE imesema ina ushahidi wa kaburi la halaiki limepatikana katika mji wa Izyum, ambao uko kaskazini-mashariki baada ya kukomboa kutoka vikosi vya Russia.

Mkuu wa polisi wa eneo hilo Volodymyr Tymoshko aliambia BBC kuwa zaidi ya miili 400 inadhaniwa kuzikwa humo.

"Russia inaacha kifo kila mahali," alisema Rais Volodymyr Zelensky, akilenga kugundulika makaburi mengine ya halaiki.

Ukraine na washirika wake wa Magharibi hapo awali walishutumu wanajeshi wa Russia kwa uhalifu wa kivita, lakini Russia imekanusha.

Bado haijabainika ni nini kilitokea kwa waathiriwa, lakini baadhi ya ushuhuda umedokeza kwamba huenda wengi walikufa kutokana na milipuko ya mabomu na ukosefu wa huduma za afya.

Pia, kuna dalili kwamba baadhi ya makaburi yanaweza kuwa ya askari wa Ukraine.

Tymoshko alisema uchimbaji wa kutoa miili utaanza Ijumaa ili kupata picha kamili ya idadi ya waathirika katika jiji hilo, ambalo lilikuwa chini ya Russia kwa zaidi ya miezi mitano.

Na katika hotuba yake mwishoni mwa Alhamisi, Rais Zelensky, alisema habari za wazi zaidi, zilizothibitishwa zingewasilishwa jana kwa waandishi wa habari wa Ukraine na wa kigeni.

"Tunataka ulimwengu kujua nini kinatokea na nini kazi ya Russia ambayo imesababisha. Bucha, Mariupol na sasa, kwa bahati mbaya Izyum," alisema.

Kiongozi huyo wa Ukraine alikuwa akizungumzia makaburi ya watu wengi yanayodaiwa kupatikana huko Bucha, karibu na mji mkuu wa Kyiv, na pia karibu na Mariupol bandari kuu ya kusini-mashariki mwa nchi hiyo ambayo sasa inakaliwa na wanajeshi wa Russia.

Andriy Yermak, mkuu wa ofisi ya Rais Zelensky, alituma picha ya kaburi hilo linalodaiwa kuwa la halaiki, pia akisema taarifa zaidi zinatarajiwa kupatikana.

**BBC**

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## CRANE FOR SALE

**30** Ton Coles Crane with **112** Feet boom and **145** feet extension.
Crane is in working condition but need some repair to put it in best shape. Going cheap only for 32 million based (exclusive VAT) on as it is where it is.

**Please contact: 0687 512244.**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**YVONNE KAFURA KATARAIYA** anatangaza kupotea kwa kadi ya gari aina ya **TOYOTA VITZ** yenye usajili namba **T799 DEF, CHASSIS NAMBA:SCP905014925 na ENGINE NAMBA: 2SZEAA4925.** Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.

**POLISI TAARIFA: DAR/OST/RB/367530/2022**

**FORM 58**
**IN THE DISTRICT COURT OF TEMEKE**
**AT ONE STOP CENTRE**
**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO 818 OF 2022**
**In the matter of the estate of the late KAGERE THOMAS MUKARARO**
**And**
**In the matter of Application for Letters of Administration by GLADYS DAUDI TANDILA**

**GENERAL CITATION**
**(Rule 75)**

All persons claiming to have any interest in the estate of the above-named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of probate ( or letters of administration) is made to the above-named petitioner.
Objections to the grant should be filed on or before the 10th day of OCT 2022
**Dated at DAR ES SALAAM this 07 day of SEPT 2022**

Registrar/Senior Resident Magistrate

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

Ndugu **PASCAL STANLAUS MACHANGO** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari aina ya **SUZUKI CARRY** yenye namba za usajili **T.796 CRG.** Yenye Chassis Na. **DD51B303777**
Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi.

**Taarifa Polisi: TAN/RB/366813/2022**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

Ndugu **HABIBA ISSA SELEMAN** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari aina ya **TOYOTA CARINA** yenye namba za usajili **T.429 CZG.** Yenye Engine namba **5AJ116072** na Chassis namba **AT2120090408**
Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi.

**TaarifaPolisi: TAN/RB/366816/2022.**

## KUPOTEA KWA CHETI



**ROYNOLD MARTIN KASHUMBA** anatangaza kupotea kwa cheti cha **KIDATO CHA NNE** chenye **INDEX NAMBA S5177-0022** kilichotolewa na baraza la mitihani la taifa kupitia **COMPASSION SECONDARY SCHOOL** mwaka **2014.** kwa yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi.

**TAARIFA YA POLISI: DSM/PHQ/RB/366560/2022**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**OFISI YA RAIS**
**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**
**HALMASHAURI YA MANISPAA MOROGORO**
**SHERIA YA UMILIKISHAJI WA ARDHI YA MWAKA 1999**
**KUPOTEA KWA BARUA YA TOLEO YA KUMILIKI ARDHI**
**BARUA YA TOLEO YENYE KUMB. NA. B.3/77/43**
**MMILIKI ALIOANDIKISHWA: CHARLES M. MICHAEL WA S.L.P 158, MOROGORO**
**ARDHI: KIWANJA NA. 77 KITALU B.3 KIWANJA CHA NDEGE MANISPAA YA MOROGORO**
**MUOMBAJI: BONIFACE FORTUNATUS KIWALE**
**MSIMAMIZI WA MIRATHI YA NDUGU CHARLES MDETE MICHAEL S.L.P 1953, MOROGORO**

Taarifa inatolewa kwamba **BARUA YA TOLEO YA KUMILIKI ARDHI** iliyotajwa hapo juu imepotea na ninakusudia kutoa **NAKALA HALISI YA BARUA YA TOLEO YA KUMILIKI ARDHI** iwapo hakuna pingamizi litakalo tolewa kwa muda wa SIKU 30 toka tarehe ya taarifa hii itakapotangazwa katika gazeti.
**HATI YA BARUA HALISI YA TOLEO** ikionekana, irudishwe kwa **MKURUGENZI WA MANISPAA-MOROGORO S.L.P166 MOROGORO**

Valency H.K
KNY: MKURUGENZI WA MANISPAA MOROGORO

**JAMHURI YAMUUNGANO WA TANZANIA**
**KATIKA BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA**
**WILAYA YA GEITA**
**MAOMBI NA 29/2022**
**MOSES KASWAHILI......MLETA MAOMBI**
**DHIDI YA**

- **SAID KHAMIS MAKINDI**
- **AGNES HALALI MAHUNDI...WAJIBU MAOMBI**

**TANGAZO LA KUITWA SHAURINI**

**Kwa AGNES HALALI MAHUNDI p**opote ulipo unafahamishwa kwamba mwombaji tajwa hapo juu amefungua shauri la madai dhidi yako katika baraza la Ardhi na nyumba wilaya Geita, maombi haya yamepangwa tarehe **20/09/2022** kwa ajili ya kutajwa/ kusikilizwa katika ofisi za baraza saa **03:00 Asubuhi.**
Hivyo basi unaamriwa kufika shaurini wewe mwenyewe au wakili wako au mtu yeyote aliye ruhusiwa kisheria. Nakala za madai zinapatikana katika ofisi za baraza.
**KAA UKIJUA** kwamba kushindwa kufika kwako, baraza litasilikiza shauri na kutoa hukumu/ maamuzi bila wewe kuwepo.
Imetolewa nami kwa Amri yangu na chapa ya baraza hili leo tarehe **01/09/2022.**

**KNY: ASHA RAJABU MASAO**
**MWENYEKITI**
**01/09/2022**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**SHABANI SEIF KAPELLA** Anatangaza kupotelewa kwa kadi ya gari **(ISUZU)** yenye usajili wa namba **T446BRR ,CHASSIS NO: NHR69E7429211.**Kwa yeyote atakaeiona au kuokota atoe taarifa kituo chochote cha polisi au piga simu namba **0756965252.**

**TAARIFA YA POLISI: MOR/MOR/RB/368745/2022.**

*Uza, Chenye Thamani Kubwa Kwa Kutangaza Nasi Kwa Bei Poa Tupigie 0782253676*

**OFISI ZA MATANGAZO MIKOCHENI INDUSTRIAL AREA, PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM.**
**MOB: +255 - 0782253676**




**TAHADHARI:** Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji **THE GUARDIAN LIMITED** hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

# HADITHI

MGENI wa ajabu atatokea kwenye kijiji cha Semwanza, Lugoba mkoani Pwani. Anakotoka hakujulikani. Watu wote wanamwogopa. Ni kwa sababu hawamjui. Msichana Siwatu anajitolea kumsaidia mgeni huyo. Kwa kufanya hivyo, anabezwa kwa maneno mengi ya kejeli kwa kumsaidia mtu asiyemjua ambaye anaweza kuwa hatari kwa kijiji. Baadhi ya viongozi wa kijiji waliungana na wanakijiji kutaka wamtimue mgeni huyo asiyejulikana, lakini akakataa katakata. Pamoja na kutishwa kuwa atatengwa na kijiji, bado msichana huyo alisimama na msimamo wake uleule wa kumsaidia kwa sababu alikuwa na shida kubwa.

Matokeo haya, yanamuingiza Siwatu kwenye msukosuko mkubwa ambao hajawahi kuupata kwenye maisha yake kiasi cha kumkatisha tamaa. Fuatilia kisa hiki.

## Kama ipo, ipo tu-23

Na Adam Fungamwango, (0716 350534)

“Basi basi usiendelee...” Ilikuwa ni sauti ya Siwatu. Hapo sasa alishajua kuwa huko mwisho hao wasichana watatu mmoja ni yeye, na aliyekuja baadaye na kumfanyia hayo yote ni yeye. Ndicho alichokifanya siku ile alipoiona sura yake kwa mara ya kwanza. Na ndicho kisa cha kukutana, akaishi kwao kwa miezi mitatu kabla ya kuondoka.

“Usiwe unasimulia kisa hicho, huwa unanipa simanzi sana mpenzi wangu.” Bakari alifarijika mno kuitwa mpenzi.

“Hapana nimesimulia na mimi baada ya mleta barua kusimulia ya kwake, sasa utapima mwenyewe nani zaidi. Aliyeandika au aliyesimulia. Aliyeandika kaandika vizuri zaidi na aliyesimulia, hadi mwenyewe machozi yanakulenga...”

Sauti za hodi zikasikika. Hazikuwa ngeni. Ni Dibwela kaka yake Siwatu, Dibwela na Billy.

Walipoingia Siwatu, bado aliendelea kushangaa kwa sababu aliambiwa kuwa ndiyo muda ambao mchumba wake atawasili. Ilikuwa ni saa 12:00 jioni.

Hilo lilimpa faraja kwa mbali Siwatu kuona sasa anaweza kughairi kuolewa na mtu huyo, badala yake kwa mtu anayempenda Bakari.

“Yuko wapi mtu mwenyewe?” Akauliza kwa ukali. Alikuwa na maana yake. Alianzishe na kuuvunja uchumba wenyewe.


“Usiwe na wasiwasi bibie, mchumba wako yuko nje hapo, tumemuacha amengia msalani, anakuja sasa hivi.” Akajibu Billy na kufanya Siwatu kunywea. Alichotaka sicho.

“Jamani sasa leo hii kila kitu kimetimia, tunakuja kumtambulisha rasmi bwana harusi mtarajiwa na wote mlio ndani humu mtafurahi.” Akanyamaza kidogo kuwaangalia Dibwela, Bakari na Siwatu ambao nyuso zao zilionekana na kama hazijakunjuka.

“Dibwela kaka wa bi harusi mtarajiwa, pamoja na kaka mwingine kama tulivyotambulishwa, pamoja na bi harusi, leo ni siku ya furaha sana, siku itakayoingia kwenye historia ya mioyo yenu wote kwa ujumla. Bila kupoteza muda sasa bwana harusi anaingia na namtambulisha kwenu.” Wote waliokuwa humo ndani wakaangalia mlangoni ili kumuona bwana harusi huyo mtarajiwa ambaye alikuwa hajaonekana hata siku moja.

Karibia dakika moja nzima kila mmoja alikuwa kimya kuangalia huyo ambaye ataingia.

“Namuomba bwana harusi mtarajiwa asimame.” Billy akamaliza ukimya. Hii




**“Ndiyo, na hayo yalikuwa na maelekezo yake, nadhani yeye alifanya hivyo kwa sababu zake ambazo mwenyewe baadaye atazieleza. Sisi tulikuja hapa tulitumwa na yeye, halafu baadaya ya siku chache akaja hapa hapa na kukaa hapa hapa. Hii sisi kutoka na kurudi kusema ana udhuru, ilikuwa ni kwa maelekezo yake.” Daudi alizidi kuwashangaza.**

iliwashtua wote waliokuwa ndani. Walikuwa wanaangalia mlangoni. wameambiwa bwana harusi yuko msalani, lakini sasa wamegeuzia kibao anaambiwa asimame.

“Ameingia saa ngapi?” Siwatu alianza kujiuliza. Alidhani anaota na kuona huenda ameingia lakini hajamuona.

“Yuko wapi huyu bwana harusi mwenyewe?” Akaendelea kujiuliza. Lilikuwa ni swali lililokuwa linaulizwa na baadhi ya watu wengine humo ndani.

Ulikuwa ni kama mchezo wa kuigiza, tena ule wa ucheshi, wenyewe wanaita komedi. Aliyesimama ni Bakari.

“Nini?” Siwatu akajiuliza. Akataka kusema kwa nguvu lakini sauti haikutoka.

“Mabibi na mabwana, huyo ndiye bwana harusi mtarajiwa ambaye siku zote hizi tulikuwa tunasema kuwa atakuja, lakini alikuwa na udhuru.”

Ilionekana kama kichekesho, lakini ukawa pia ni mshangao. Siwatu yeye ilikuwa bado kidogo azimie. Alikuwa kama anaota ndoto ambayo haielewi.

“Unajua hili suala hatulielewi. Huyu Bakari si alikuwa yupo hapa hapa, na nyinyi mkasema mnakwenda kumchukua bwana harusi, imekuwaje ikawa ndiyo huyu huyu ambaye mara mbili mnakuja mnamkuta?” Ilibidi Dibwela aulize ili apate ukweli kwani ilionekana kama vile Billy na Daudi wanawachezea shere.

Daudi akaamua kumsaidia Billy ambaye kwa muda mrefu alikuwa anaongea yeye.

“Samahani shemeji Dibwela, tangu tulipokuja hapa kukusaka kukuambia kuwa tumeleta barua, bosi wetu anataka kumuoa dada yako, basi bosi mwenyewe ni huyu hapa Bakari na si mwingine.”

“Kwa hiyo hizi mara mbili mlipokuwa mnakuja mnaniuliza ni nani kana kwamba hamjui, kumbe ni yeye?” Dibwela aliuliza tena.

“Ndiyo, na hayo yalikuwa na maelekezo yake, nadhani yeye alifanya hivyo kwa sababu zake ambazo mwenyewe baadaye atazieleza. Sisi tulikuja hapa tulitumwa na yeye, halafu baadaya ya siku chache akaja hapa hapa na kukaa hapa hapa. Hii sisi kutoka na kurudi kusema ana udhuru, ilikuwa ni kwa maelekezo yake.” Daudi alizidi kuwashangaza.

Wakati wote huo ni kama Siwatu alikuwa amechanganyikiwa. Haelewi nini kimetokea. Akadhani yote yake siyo kweli, labda anaota. Hivi ni kweli hayupo huyo mtu, ila ni Bakari. Bakari yeye huyu aliyeishi naye miezi mitatu, akaondoka na kukaa huko mwaka mzima na aliporudi ndiyo akamwambia anataka amuoe, wakati huo akiwa ameshamkubali mtu mwingine. Kumbe mtu mwingine huyo ni yeye pia. Kilikuwa ni kitu ambacho kwenye maisha yake hakikutarajia na kilikuwa kigeni. Lakini bado akawa na maswali mengi juu ya usahihi na hilo.

“Jamani kwani hili likoje, mimi naona mnanichanganya tu.” Ilikuwa ni sauti kali iliyosikika ghafla. Alikuwa ni Siwatu ambaye alionekana amechukia hivi, lakini akiwa kama amehamanika na kukosa nguvu. Sauti hiyo ilimjia ghafla baada ya muda mrefu wa kushindwa hata kuongea.

“Kwanza kabisa naomba samahani kwa haya yaliyotokea. Ni kwamba itafika mpaka mwisho wa dunia hamtoweza kumuona mchumba ambaye anatajwa kuwa angekuja kumuoa Siwatu. Huyu mchumba ni mimi. Na hata barua ambayo Siwatu ulikuwa unaisoma ukidhani kuwa imeandikwa na huyo mtu, iliandikwa na mimi mwenyewe. Hata ukiunganisha mkasa uliousoma utagundua kuwa unafanana na ule niliokusimulia baada ya kukupora barua na kuanza kusimulia mimi mwenyewe. Kifupi mkasa ni huo huo mmoja. Ila kwenye barua ulikuwa umeandikwa na baadaye mimi nilianza kusimulia pale ulipoishia kwenye barua, ndiyo maana unaona ulifanana sana. Kisa ulichokisoma kwenye barua tangu mwanzo ni changu mimi na ndicho kilichosababisha mpaka nitupwe hapa kijijini kwenu na wewe kuniokoa.” Akasema Bakari na kusababisha mshangao kwa Dibwela na Siwatu.

Kifupi ni kwamba Billy na Daudi walijua kila kitu. Na kila walichokifanya kilitokana na maelekezo ya Bakari.

“Nilifanya yote haya kwa sababu zangu ambazo nitazisema mbele ya safari. Kwa kifupi tu mimi jina langu kamili naitwa Samson Dau na si Bakari. Jina la Bakari lilitunga mwenyewe ili litumike hapa kijiji wakati ule nilipookolewa na Siwatu. Sikutaka kujitaja kwa jina langu halisi kwa sababu zangu binfasi.”

Mpaka hapa, tayari Siwatu akili yake ilishaanza kukaa sawa, na kutambua yule mtu aliyeishi naye baada ya kumuokoa aliyemtambua kwa jina la Bakari, ndiye Samson Dau au Bosi Mulango kama Billy na Daudi walivyopenda kumwita.

“Kama nilivyoandika kwenye barua iliyosomwa na Siwatu mimi nimetoka kwenye familia ya kitajiri, na hawa mnaowaona hapa ni baadhi ya mamia ya wafanyakazi wangu. Pia makazi yangu siyo Chalinze kama nilivyosema wakati ule ila ni Dar es Salaam. Yote nilifanya kwa mkakati maalum wa kujilinda mimi mwenyewe na kuna vitu nilikuwa nahitaji kufanya uchunguzi kabla ya kuvithibitisha.”

ITAENDELEA JUMAMOSI

# KMKM, KIPANGA ZAAHIDI MAKUBWA MICHUANO CAF

**Na Hawa Abdallah, ZANZIBAR**

WAWAKILISHI wa Zanzibar katika mashindano ya kimataifa, KMKM na Kipanga, zimeahidi kusaka matokeo mazuri katika mechi za marudiano watakazocheza leo visiwani hapa, imefahamika.

Kipanga, ambao ni mabingwa wa Kombe la Shirikisho Zanzibar watashuka dimbani kuanzia saa 10:00 jioni kuwakaribisha Al Hilal Wau kutoka Sudan Kusini wakati KMKM yenyewe itawavaa Al Ahli Tripoli kuanzia saa 3:00 usiku.

Akizungumza na gazeti hili jana, Kocha Msaidizi wa Kipanga, Khamis Hassan, alisema wamejiandaa kupata ushindi katika mchezo huo ili wasonge mbele katika michuano hiyo.

Hassan alisema wachezaji wake wote wapo vizuri na tayari kupambana ili kuhakikisha wanatimiza malengo yao ya kutinga hatua ya pili.

"Tunahitaji kupata ushindi ili kutimiza lengo la kuvuka hatua hii ya awali,lakini pia kuweka historia kwa timu za Zanzibar kuondolewa mapema katika michuano hii ya kmataifa," alisema Hassan.

Nahodha wa Kipanga, Ibrahim Imran, alisema wachezaji wote wako katika hali nzuri na wana ari ya kukakikisha wanawaondoa Wasudani wao.

"Tunatarajia kupambana ili kuhakikisha ushindi unapatikana, tutafuata maelelezo yote tuliyopewa na walimu wetu hatimaye kuvuka hatua hii tena tukiwa kwenye uwanja wa nyumbani," Imran alisema.

Naye Kocha Mkuu wa Al Hilal FC Wau, Hamad Abdi Elrahman, alisema mchezo huo wa marudiano utakuwa mzuri na mgumu kwa sababu timu zote zina nafasi ya kusonga mbele katika michuano hiyo.

Elrahman alisema licha ya kucheza ugenini hana wasiwasi na mchezo huo huku akifurahia hali ya usalama na amani iliyoko Zanzibar.

"Najua utakuwa mchezo mazuri na mgumu, sisi wote tunasaka matokeo, mechi ya kesho (leo), itaamua nani anavuka hatua hii, hivyo matumaini yangu utakuwa mchezo wa kasi na wenye uhitaji kwa wote," alisema kocha huyo.

Katika mechi ya kwanza Kipanga ilitoka sare ya bao 1-1 dhidi ya Al Hilal Wau wakati KMKM ilifungwa magoli 2-0 na Al Ahli Tripoli.




Ofisa Mtendaji Mkuu wa Benki ya NMB (CEO), Ruth Zaipuna (kulia), akimkabidhi vifaa vya michezo Mwenyekiti wa Bunge SC,Tarimba Abbas (katikati) kwa ajili ya timu yao itakayoshiriki bonanza la Kivumbi na Jasho. Kushoto ni nahodha wa timu ya kikapu, Stanslaus Nyongo na Makamu Mwenyekiti wa Bunge SC, Ester Matiku. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# NMB, Bunge SC hapatoshi leo

**Na Mwandishi Wetu, DODOMA**

MSIMU wa pili wa bonanza la 'NMB Kivumbi na Jasho,' linalokutanisha timu za michezo mbalimbali za Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Benki ya NMB, linaunguruma leo jijini hapa, hii ni baada ya jana benki hiyo kuikabidhi Bunge SC vifaa vya michezo vyenye thamani ya Sh. milioni 20.

Kivumbi na Jasho ni bonanza linalolenga kujenga na kuimarisha mahusiano mema baina ya Bunge na NMB, ambapo Bunge SC imeahidi kulitumia vyema kama ilivyofanya msimu uliopita kuzipa makali timu zao zinazojiandaa na Mashindano ya Mabunge kwa nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki (EALA 2022).

Mwenyekiti wa Bunge SC, Tarimba Abbas, alisema, wanalichukulia kwa uzito mkubwa tukio la leo, na kuwa kwao Kivumbi na Jasho ni zaidi ya bonanza.

"Tunatambua na kuthamini malengo ya bonanza hili, lakini tuwe wazi kwetu ni zaidi ya hapo. Mwaka Jana lilitupa kipimo sahihi kuelekea EALA 2021, ambako tuliibuka washindi wa jumla katika michezo nane tuliyoshiriki. Tunatarajia kurejea mafanikio hayo mwaka huu kupitia bonanza hili," alisema Tarimba.

Ofisa Mtendaji Mkuu wa NMB, Ruth Zaipuna, awali aliushukuru uongozi wa Bunge SC na manahodha wa timu za michezo yote kwa kuipa nafasi benki hiyo kuendelea na msimu wa pili wa bonanza hilo, ambalo hubeba fursa mbalimbali sio tu kwa Bunge, bali taasisi nyingine za serikali.

"Bonanza litaanza saa 12 asubuhi kwa matembezi yatakayoanzia Viwanja vya Bunge hadi Chinangali Park itakochezwa michezo mbalimbali, kuthibitisha faida za bonanza hili, tukifika pale tutakabidhi vifaa kwa ajili ya Hospitali ya Uhuru, vyenye thamani ya Sh. milioni 50 na baada ya hapo, ndipo Kivumbi na Jasho kitakapoanza," aliongeza ofisa huyo.

## Ngome yaitamani Ligi Kuu Zanzibar

**Na Hawa Abdallah, ZANZIBAR**

BAADA ya timu yake kupata ushindi katika mechi mbili walizocheza, Kocha Mkuu wa Ngome FC, Khamisi Ame, amesema malengo yake ni kuona anapanda daraja na kushiriki Ligi Kuu Zanzibar kwenye msimu ujao wa 2023/2024.

Mbali na Ngome FC, timu nyingine zenye pointi sita katika Ligi ya Kanda ya Unguja ni pamoja na vinara New City na Umoja wa Mbuzini FC.

Ame alisema timu yake tayari imeshakuwa na uzoefu wa ligi hiyo na msimu huu wamejipanga kuhakikisha anakipandisha kikosi hicho.

"Msimu huu tunataka kuondoka katika hili daraja, japo ni mapema kusema hivi,lakini haya ndio malengo yetu makuu, tunataka kubadili jina la Wafalme wa Kanda na twende Ligi Kuu," alisema Ame.

Timu ambazo zimeshindwa kuvuna pointi katika ligi hiyo ya Kanda ambayo kila klabu imecheza michezo miwili mpaka sasa ni New Boys, Gulioni na Strong Fire wakati New King ina pointi moja.

## Mzunguko wa 2 wavu Jumanne

**Na Shufaa Lyimo**

MZUNGUKO wa pili wa Ligi ya Taifa ya Wavu imepangwa kufanyika kuanzia Septemba 20 hadi 24, mwaka huu kwenye Uwanja wa Ndani wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam.

Katibu Msaidizi wa Chama cha Wavu Tanzania (TAVA), Shukuru Ally, alisema maandalizi ya ligi hiyo inayoshirikisha timu 20 kutoka mikoa mbalimbali yanaendelea vizuri.

"Ligi hii itashirikisha timu nane za wanawake na wanaume watawakilishwa na timu 12, tunaomba mashabiki wajitokeze kwa wingi katika mashindano haya," alisema Ally.

Kiongozi huyo alisema timu nne za juu zitakazofanya vizuri zitapata nafasi ya kushiriki mzunguko wa tatu utachezwa kuanzia Oktoba 2 hadi 6, mwaka huu hapa jijini.

Alitaja mikoa iliyoleta timu ni pamoja na Tabora, Iringa, Arusha, Dodoma, Pwani na Kilimanjaro.

## ZISIKUPITE

### BELLINGHAM AKARIBIA LIVERPOOL

KLABU ya Liverpool inaongoza katika kinyang'anyiro cha kumpata kiungo wa kati wa Borussia Dortmund na Timu ya Soka ya Taifa ya England, Jude Bellingham mwenye umri wa miaka 19, dhidi ya Manchester United .***(Telegraph)***

### LIVERPOOL YAMTAJA NUNES

LIVERPOOL wanafikiria kumnunua kiungo wa Wolves na Timu ya Taifa ya Ureno, Matheus Nunes mwenye umri wa miaka 24 kama watamkosa Jude Bellingham. ***(UOL, via Mirror)***

### ZIYECH ALITAKA KUONDOKA

WINGA wa Chelsea, Hakim Ziyech mwenye umri wa miaka 29, alikuwa na nia ya kuondoka Stamford Bridge msimu huu wa joto, huku klabu za Ajax na AC Milan zikimhitaji mchezaji huyo wa kimataifa wa Morocco kurejea. ***(Football.London)***

### LEAO ALITAKIWA CHELSEA

CHELSEA pia walimtaka mshambuliaji wa AC Milan na Ureno, Rafael Leao mwenye umri wa miaka 23, wakati wa dirisha la joto kwa mujibu wa Mkurugenzi wa klabu hiyo, Paolo Maldini. ***(FourFourTwo)***

### FREUND ANUKIA CHELSEA

MKURUGENZI wa Mchezo wa Red Bull Salzburg, Christoph Freund, amekataa kufuatilia uwezekano wa kujiunga na Chelsea katika jukumu kama hilo, na kusema The Blues walionyesha nia ya kumnunua mshambuliaji wa klabu ya Austria na Slovenia, Benjamin Sesko mwenye umri wa miaka 19, wakati wa majira ya joto. ***(Sky Austria, via 90 Min)***

### CAICEDO KUICHEZEA ECUADOR

KIUNGO wa kati wa Brighton, Moises Caicedo, mwenye umri wa miaka 20, amesema analenga kuichezea Ecuador katika fainali za Kombe la Dunia zitakazofanyika baadaye mwaka huu. ***(Ole, via 90 Min)***

### MUDRYK AGEUKA LULU

KLABU ya Newcastle United wanavutiwa na winga wa Shakhtar Donetsk na Timu ya Taifa ya Ukraine, Mykhaylo Mudryk, mwenye umri wa 21, ambaye pia amekuwa akihusishwa na Arsenal na Brentford. ***(Football Insider)***

### DIAZ AGOMBEWA ULAYA

KLABU za Valencia, Villarreal, Celta Vigo na Real Sociedad zinapanga ofa za kabla ya mkataba wa awali kwa mshambuliaji wa Blackburn Rovers na Chile, Ben Brereton Diaz, huku Everton na Leeds United pia zikimlenga mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 23. ***(Football Insider)***

### POGBA MASHAKANI UFARANSA

KOCHA wa Ufaransa, Didier Deschamps amesema hatamwita kiungo wa kati wa Juventus, Paul Pogba, ambaye amefanyiwa upasuaji wa goti, katika kikosi chake cha Kombe la Dunia hadi mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 29 atakapokuwa sawa kabisa. ***(Mirror)***

### HAG KUPEWA KITITA

KOCHA wa Manchester United, Erik ten Hag atapewa takribani pauni milioni 70 za kutumia katika dirisha la usajili la Januari na kiasi hicho kinaweza kuongezeka iwapo mshambuliaji wa Ureno, Cristiano Ronaldo mwenye umri wa miaka 37 ataondoka hapo Old Trafford. ***(Sun)***

## DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# HAG : UBORA WA RONALDO UTAREJEA

**Asema mshambuliaji huyo atarudi katika kiwango chake baada ya kuonyesha...**

**MANCHESTER, England**

KOCHA wa Manchester United, Erik ten Hag, amedai mshambuliaji, Cristiano Ronaldo, amejitolea kabisa kwa ajili ya klabu hiyo ya Old Trafford.

Ronaldo alijaribu kuondoka katika klabu hiyo msimu huu wa joto kutokana na kutaka kucheza kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya lakini alishindwa.

Kuanza kwake dhidi ya Sheriff, katika mechi ya Ligi ya Europa juzi ilikuwa ni mara yake ya tatu katika mashindano yote hadi sasa, na alifungua akaunti yake ya mabao chini ya Ten Hag kwa penalti wakati wakiibuka na ushindi wa magoli 2-0.

Ten Hag, ameapa kufanya kazi na Ronaldo ili kumfanya aongeze kasi baada ya muda wake mfupi wa kujiandaa na msimu mpya na alimsifia sana mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 37 baada ya kuonyesha kiwango kizuri dhidi ya Sheriff.

"Ni kweli yuko karibu, atakapoimarika zaidi atafunga zaidi," Hag alisema kuhusu Ronaldo.

"Amejitolea kabisa kwa mradi huu, anahusika kabisa, pia ana muunganisho unaokuja karibu naye na anaunda miunganisho kwa hivyo ninafurahia hilo."

Baadaye, Ten Hag alikiri kufunga bao lake la kwanza kwenye kampeni kunaweza kumfanya kurejea katika kiwango chake.

"Ronaldo alihitaji bao hilo," alisema Ten Hag akiiambia MUTV.

"Mara nyingi alikuja karibu, lakini alitaka sana. Tuna furaha kwake na timu ilitaka kumletea bao.

"Unajua Cristiano atafunga penalti."

SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!

SUPA JACKPOT KWA 1000/- 1,031,2

MECHI KALI
WOLVERHAMPTON
VERSUS
MANCHESTER CITY
1 | 7.41
X | 4.82
2 | 1.36

KUWEKA PESA:
- PIGA *150*87#, CHAGUA 4
- WEKA PESA.
tigo pesa
vodacom m-pesa
airtel money
EZYPESA
SEND

SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
PIGA *150*87#
GBT:0249 HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, PIGA:
0764115588, 0677115588
0685115588
18+
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa

# TONEY, HENDERSON WAITWA KUIVAA ITALIA, UJERUMANI



**LONDON, England**

KOCHA Mkuu wa Timu ya Soka ya Taifa ya England, Gareth Southgate, ametaja kikosi chake cha wachezaji 28 kwa ajili ya mechi za kimataifa za kirafiki zitakazochezwa Septemba hii, huku Ivan Toney akiitwa kwa mara ya kwanza.

Mshambuliaji huyo wa Brentford hajawahi kuichezea England na sasa atapata nafasi ya kuikabili Italia ugenini na dhidi ya Ujerumani nyumbani katika michuano ya Ligi ya Mataifa ya Uefa.

Jarrod Bowen, ameanza msimu huu polepole akiwa West Ham, lakini amebakiza nafasi yake kwenye kikosi baada ya kucheza kwa mara ya kwanza katika kikosi cha England msimu wa joto, huku Marc Guehi wa Crystal Palace akirejea pia.

Huku Jordan Pickford akiwa ameumia, Dean Henderson amerejea katika kikosi hicho baada ya kucheza kwa mkopo Nottingham Forest.

Kikosi kamili cha England.

Makipa: Nick Pope (Newcastle United), Aaron Ramsdale (Arsenal) na Dean Henderson (Nottingham Forest) wakati walinzi ni Reece James (Chelsea), Trent Alexander-Arnold (Liverpool), Kieran Trippier (Newcastle United), Kyle Walker (Manchester City, Harry Maguire (Manchester United), Fikayo Tomori (AC Milan), John Stones (Manchester City), Marc Guehi (Crystal Palace), Conor Coady (Everton), Eric Dier (Tottenham Hotspur), Luke Shaw (Manchester United) na Ben Chilwell (Chelsea).

Viungo walioitwa ni Declan Rice (West Ham United), Jude Bellingham (Borussia Dortmund), Mlima wa Mason (Chelsea), Kalvin Phillips (Manchester City) na James Ward-Prowse (Southampton) na washambuliaji wataongozwa na Harry Kane (Tottenham Hotspur), Tammy Abraham (AS Roma), Ivan Toney (Brentford), Raheem Sterling (Chelsea), Phil Foden (Manchester City), Bukayo Saka (Arsenal), Jarrod Bowen (West Ham United) na Jack Grealish (Manchester City).

## Bellingham azigonganisha Liverpool, United

**LONDON, England**

KLABU za Liverpool na Manchester United zimeingia kwenye mbio moja kuwania saini ya Jude Bellingham, kwa mujibu wa The Telegraph.

Mkataba wa kiungo huyo wa kikosi cha Timu ya Soka ya Taifa ya England katika klabu yake ya Borussia Dortmund unamalizika 2025.

Bellingham, aliondoka Uingereza alipohama kutoka Birmingham City kwenda Dortmund mwaka 2020.

Hata hivyo, kwa mujibu wa ripoti hiyo, Liverpool ndio wanaongoza katika mbio za kumsajili kinda huyo.

United, pia wanavutiwa na mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 19, ambaye ameanza mechi zote tisa za Dortmund msimu huu.

Bellingham, anaweza kuruhusiwa kuondoka Borussia Dortmund mwaka 2023, na klabu hiyo ya Ujerumani inatarajia kupokea ofa yoyote.



## HABARI MICHEZO

43,893/-

# KISINDA AIPA JEURI YANGA BARA, CAF

**Na Adam Fungamwango**

KLABU ya Yanga imefurahishwa na uamuzi wa kuruhusiwa kwa winga wake waliomsajili kutoka RS Berkane ya Morocco, Tuisila Kisinda, kucheza Ligi Kuu Tanzania Bara na mashindano ya kimataifa ya Ligi ya Mabingwa Afrika, ikisema uwepo wake utaongeza 'kitu kikubwa' kwenye kikosi chao.

Kisinda, amepata leseni ya kuanza kuitumikia Yanga baada ya klabu hiyo kumhamisha nyota mwingine wa kigeni Mzambia, Lazarous Kambole kuelekea Wakiso Giants ya Uganda.

Meneja wa Yanga, Walter Harrison, alisema jana mara baada ya kupata uamuzi kutoka katika Kamati ya Sheria na Hadhi za Wachezaji ya Shirikisho la Soka Tanzania (TFF), klabu na wachezaji wenzake walifurahishwa na hii inaonyesha jinsi gani walikuwa wanamhitaji.

"Ni jambo jema ambalo kila shabiki wa Yanga alitamani litokee, hatimaye limetokea baada ya sintofahamu. Kila mtu hapa kambini amefurahi na wamesema wako tayari kushirikiana naye, kila mchezaji amefurahi," alisema Harrison.

Meneja huyo alisema hata wakati ambapo alikuwa amezuiwa, Kisinda alikuwa anafanya mazoezi ya nguvu na yuko tayari kuwapa mashabiki mazuri ambayo wameyazoea kutoka kwake.

"Tunasubiri kuona jinsi gani atapata nafasi, amekuwa akifanya yale yale ambayo wengi wamezoea kuyaona, lakini sasa wanachama na mashabiki wa Yanga wanataka kuona hayo yakitokea uwanjani, nafasi hiyo imepatikana, ujio wake utaongeza kitu kwenye kikosi chetu," alisema meneja huyo.

Awali Yanga, ilimsajili Kisinda kutoka AS Vita ya Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC).

TFF iliizuia Yanga kumtumia Kisinda kwa sababu tayari ilishawasilisha majina 12 ya wachezaji wa kigeni kama kanuni zinavyosema.



Kikosi cha Timu ya Soka ya Taifa ya Watu wenye Ulemavu (Tembo Warriors), pamoja na viongozi wao baada ya kufika Uturuki ambapo wameweka kambi kujiandaa na fainali za dunia zitakazofanyika kuanzia wiki ijayo nchini humo. **PICHA: BMT**

# Nape ataja tuzo mpya ya filamu

**Na Mary Geofrey**

WAZIRI wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Nape Nnauye, ameishauri Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA) kuandaa tuzo ya Mzalishaji Bora wa maudhui ya ndani ya filamu ili kuongeza ushindani katika soko la sanaa hiyo.

Nape, pia ameitaka mamlaka hiyo kuweka kanuni ambazo zitasimamia wazalishaji binafsi wa maudhui ili kuwezesha kuuza kazi zao katika soko la nje.

Waziri huyo aliyasema hayo jana jijini, Dar es Salaam katika mkutano uliowakutanisha wadau wa uhamasishaji uandaaji na usambazaji wa maudhui bora ya filamu hapa nchini.

Aliwataka pia, wadau wa uzalishaji na usambazaji wa maudhui kuweka mikakati itakayosaidia nchi kuzalisha na kuandaa maudhui bora ya kushindana katika soko la utandawazi.

Alisema, kampuni kubwa za kimataifa zimekuwa zikishindana kutengeneza na kusambaza tamthilia na katuni za watoto, vichekesho .

Awali, Mwenyekiti wa Kamati ya Maudhui TCRA, Habi Gunze, alitaja baadhi ya changamoto zilizobainika katika uzalishaji wa maudhui ni uhaba wa mitaji, mitaala kupitwa na wakati na ukosefu wa mafunzo kwa wabunifu.

## SUPA JACKPOT
## MECHI WIKI HII
### BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01. 17/09/22 | 18:00 | Montpellier vs Strasbourg | 2.73 | 3.33 | 2.48 |
| 02. 17/09/22 | 19:00 | Spezia vs Sampdoria | 2.55 | 3.25 | 2.75 |
| 03. 17/09/22 | 19:15 | Zulte Waregem vs St. Truiden | 2.94 | 3.49 | 2.28 |
| 04. 17/09/22 | 19:30 | Valencia vs Celta Vigo | 2.35 | 3.08 | 3.18 |
| 05. 17/09/22 | 19:30 | Borussia Monchengladbach vs RB Leipzig | 2.93 | 3.57 | 2.23 |
| 06. 17/09/22 | 20:00 | PAU F vs Valenciennes | 2.72 | 3.07 | 2.77 |
| 07. 17/09/22 | 20:00 | Bastia vs Metz | 2.52 | 3.17 | 2.92 |
| 08. 17/09/22 | 20:00 | US Quevilly Rouen vs Laval | 2.47 | 3.16 | 3.01 |
| 09. 17/09/22 | 22:30 | Atlanta United vs Philadelphia Union | 2.30 | 3.61 | 2.91 |
| 10. 18/09/22 | 02:30 | New England Revolution vs Montreal Impact | 2.35 | 3.57 | 2.87 |
| 11. 18/09/22 | 13:15 | GO Ahead Eagles vs FC Emmen | 2.36 | 3.48 | 2.83 |
| 12. 18/09/22 | 14:30 | Jahn Regensburg vs St. Pauli | 2.88 | 3.62 | 2.26 |
| 13. 18/09/22 | 15:00 | Randers FC vs Silkeborg IF | 2.47 | 3.39 | 2.74 |
| 14. 18/09/22 | 15:30 | SC Heerenveen vs Twente | 2.73 | 3.58 | 2.38 |
| 15. 18/09/22 | 16:00 | Clermont Foot vs Troyes | 2.40 | 3.33 | 2.83 |
| 16. 18/09/22 | 17:30 | FC Arouca vs Vitoria Guimaraes | 2.79 | 3.19 | 2.54 |
| 17. 18/09/22 | 19:00 | FC Midtjylland vs FC Copenhagen | 2.50 | 3.40 | 2.70 |

## MECHI ZA USHINDI

"1" NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA "X" NI TIMU KUTOKA SARE "2" NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

## JUMAMOSI - 17/09/2022

| MUDA | GAME ID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 14:30 | 5182 | Wolverhampton vs Manchester City | 7.41 | 4.82 | 1.36 |
| 14:30 | 5700 | Swansea vs Hull City | 1.83 | 3.51 | 4.01 |
| 15:00 | 2099 | Mallorca vs Almeria | 2.01 | 3.23 | 3.79 |
| 16:00 | 2486 | Bologna vs Empoli | 2.08 | 3.39 | 3.29 |
| 16:30 | 3399 | Borussia Dortmund vs Schalke 04 | 1.35 | 5.20 | 6.80 |
| 16:30 | 3752 | Augsburg vs Bayern Munchen | 12.98 | 7.59 | 1.15 |
| 16:30 | 4225 | Bayer Leverkusen vs Werder Bremen | 1.62 | 4.19 | 4.49 |
| 16:30 | 5797 | Stuttgart vs Eintracht Frankfurt | 2.25 | 3.44 | 2.89 |
| 17:00 | 2667 | Luton Town vs Blackburn | 2.24 | 3.20 | 3.10 |
| 17:00 | 3204 | Newcastle vs Bournemouth | 1.43 | 4.39 | 6.59 |
| 17:00 | 3324 | Preston vs Sheffield Utd | 3.10 | 3.15 | 2.27 |
| 17:00 | 3831 | Norwich City vs West Bromwich | 2.21 | 3.40 | 3.00 |
| 17:00 | 4020 | Huddersfield vs Cardiff | 2.59 | 3.09 | 2.69 |
| 17:00 | 4159 | Burnley vs Bristol City | 1.65 | 3.81 | 4.71 |
| 17:00 | 4829 | Wigan vs Reading | 2.04 | 3.30 | 3.50 |
| 17:00 | 4847 | QPR vs Stoke City | 2.32 | 3.30 | 2.90 |
| 17:00 | 4852 | Birmingham vs Coventry | 2.79 | 3.18 | 2.46 |
| 17:00 | 4972 | Millwall vs Blackpool | 2.01 | 3.34 | 3.54 |
| 17:15 | 1999 | Barcelona vs Elche | 1.12 | 7.94 | 18.59 |
| 17:30 | 2203 | Gil Vicente vs Rio Ave | 2.00 | 3.31 | 3.66 |
| 17:30 | 3227 | Sparta Rotterdam vs Groningen | 2.14 | 3.24 | 3.29 |
| 17:30 | 5460 | Santa Clara vs Pacos Ferreira | 2.03 | 3.21 | 3.71 |
| 18:00 | 1894 | Montpellier vs Strasbourg | 2.48 | 3.31 | 2.71 |
| 18:00 | 3883 | LASK Linz vs WSG Wattens | 1.33 | 4.93 | 6.90 |
| 18:30 | 1356 | Sekhukhune United vs Stellenbosch | 2.26 | 2.70 | 3.75 |
| 19:00 | 2503 | Sport Podbrezova vs AS Trencin | 2.10 | 3.33 | 3.09 |
| 19:00 | 2506 | Odd Ballklubb vs Ham-Kam | 2.03 | 3.46 | 3.41 |
| 19:00 | 3879 | Dinamo Moscow vs Zenit St Petersburg | 5.62 | 4.21 | 1.50 |
| 19:00 | 4331 | Spezia vs Sampdoria | 2.60 | 3.15 | 2.65 |
| 19:15 | 1005 | Cercle Brugge vs Oostende | 1.75 | 3.66 | 4.31 |
| 19:15 | 2569 | Zulte Waregem vs St Truiden | 2.76 | 3.32 | 2.43 |
| 19:30 | 2166 | Monchengladbach vs RB Leipzig | 2.90 | 3.55 | 2.20 |
| 19:30 | 5103 | Valencia vs Celta Vigo | 2.35 | 3.18 | 3.03 |
| 19:45 | 2989 | Vitesse Arnhem vs FC Volendam | 1.44 | 4.68 | 5.77 |
| 20:00 | 1449 | Panetolikos vs AEK Athens | 5.45 | 3.48 | 1.65 |
| 20:00 | 1897 | New York City vs NY Red Bulls | 2.30 | 3.41 | 3.01 |
| 20:00 | 3625 | Istanbulspor vs Besiktas | 5.22 | 4.22 | 1.55 |
| 20:00 | 5742 | GD Estoril vs Porto | 9.44 | 5.22 | 1.29 |
| 21:00 | 1070 | Waalwick vs Cambuur | 2.13 | 3.49 | 3.09 |
| 21:00 | 5091 | Kaizer Chiefs vs SuperSport Utd | 2.05 | 2.91 | 4.01 |
| 21:30 | 1459 | Panathinaikos vs PAS Giannina | 1.26 | 5.01 | 12.02 |
| 21:30 | 4957 | Hamburger SV vs Fortuna Dusseldorf | 1.98 | 3.55 | 3.40 |
| 21:45 | 3060 | Charleroi vs KVC Westerlo | 2.18 | 3.46 | 3.06 |
| 21:45 | 5110 | Torino vs Sassuolo | 1.77 | 3.69 | 4.08 |
| 21:45 | 5409 | Middlesbrough vs Rotherham | 1.61 | 3.85 | 5.00 |
| 22:00 | 5025 | Athletic Bilbao vs Rayo Vallecano | 1.54 | 3.94 | 6.06 |
| 22:00 | 5814 | Lille vs Toulouse | 1.74 | 3.87 | 4.13 |
| 22:30 | 3725 | Boavista vs Sporting Lisbon | 6.23 | 4.22 | 1.48 |
| 22:30 | 4352 | Avai vs Atletico Mineiro | 4.72 | 3.59 | 1.64 |
| 22:30 | 4505 | Atlanta United FC vs Philadelphia Union | 2.45 | 3.66 | 2.64 |

CHEZA KWA WAJIBU. KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.

Michezo
Jumamosi Septemba 17, 2022
Nipashe



## Hag : Ubora wa Ronaldo utarejea

# Yanga yakamilisha mawindo ya Zalan

## ●●●Kisinda, majeruhi wapangua kikosi Jangwani, Nabi atahadharisha...

**Na Saada Akida**

IKIWA na mtaji wa mabao 4-0, Yanga wanatarajia kuwakaribisha Zalan FC kutoka Sudan Kusini katika mechi ya marudiano ya mashindano ya kimataifa ya Ligi ya Mabingwa Afrika itakayochezwa leo kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam.

Mbali na Yanga, wawakilishi wengine wa Tanzania Bara, Geita Gold FC watashuka dimbani kuwavaa Hilal Alsahil kutoka Sudan Kaskazini katika michuano ya Kombe la Shirikisho Afrika.

Hata hivyo, katika mechi ya leo, Yanga itawakosa wachezaji wake wanne ambao ni Bernard Morrison, Jesus Moloko, Djuma Shabaan na Khalid Aucho aliyeumia katika mchezo uliopita wa Ligi Kuu Tanzania Bara dhidi ya Mtibwa Sugar.

Kocha Mkuu wa Yanga, Nesreddine Nabi, alisema wamejiandaa vizuri kuelekea mchezo huo licha ya wachezaji wake kukabiliwa na uchovu lakini anaimani watapambana kutafufa matokeo mazuri.

Nabi alisema, amepanga kufanya mabadiliko katika kikosi chake kufuatia baadhi ya nyota kukosekana lakini hana wasiwasi na mchezo huo.

Kocha huyo alisema wachezaji wake ni wakubwa na kila mmoja anatambua majukumu yake kwa sababu malengo yao ni kuendelea kupata matokeo chanya na kusonga mbele katika michuano hiyo.

"Mchezo hautakuwa rahisi kwa sababu wapinzani wetu wako nchini muda mrefu na wamezoea mazingira, wachezaji wanatakiwa kujituma zaidi kutafuta matokeo mazuri hii mechi ni tofauti na ligi, lazima tushinde ili kusonga mbele katika michuano hiyo.

"Tuisila Kisinda, ni mchezaji mzuri, nimefurahi kurejea kikosini, ataongeza kitu katika timu kama atakuwa na ubora wake wa awali," alisema Nabi.

Kocha wa Zalan FC, Mawen Deng, alisema wamejiandaa vizuri na tayari ameyafanyia kazi mapungufu yaliyojitokeza katika mchezo uliopita na wamejipanga kutorudia makosa katika mechi ya leo.

"Tuko tayari kwa ajili ya mchezo wetu wa kesho (leo), kwa maandalizi tuliyofanya tunaimani ya kufanya vizuri na Yanga kuingia kwa umakini kwa sababu mechi hii haitakuwa kama iliyopita.

"Yanga ni timu kubwa tunawaheshimu lakini tumeona ubora wake, tutawachunga zaidi baadhi ya wachezaji, Mayele (Fiston)na Feisal (Fei Toto), ambao walikuwa hatari," alisema Deng.

Naye Kocha Msaidizi wa Geita Gold FC, Mathias Wandiba, alisema wamejiandaa vizuri na wako tayari kwa ajili ya kushindana ili kupata matokeo mazuri ya ushindi wa kuanzia mabao 2-0.

Wandiba, alisema walipoteza mechi ya awali kutokana na kukosa umakini, wamefanyia kazi kwa ajili ya kusonga mbele katika michuano hiyo.

" George Mpole amerejea kikosini na kufanya mazoezi na wenzake,suala la kucheza kesho (leo), ni jukumu la benchi la ufundi baada ya mazoezi ya mwisho. Malengo yetu ni kuvuka, ili kufika huko lazima tupambane tushinde katika mchezo wetu huu zaidi ya mabao 2-0 kwa ajili ya kupindua meza," alisema Wandiba.

Naye Reymond Masota, kutoka Geita Gold FC alisema wamejiandaa kwenda kupambana ili kuhakikisha wanapata matokeo mazuri na kusonga mbele katika mashindano hayo.




Wachezaji wa Yanga wakipambana kuwania mpira katika mazoezi ya timu hiyo kuelekea mechi ya mashindano ya kimataifa ya Ligi ya Mabingwa Afrika dhidi ya Zalan FC itakayochezwa leo kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam. **PICHA: MTANDAO**

## Mgunda arejesha heshima Simba SC

**Na Adam Fungamwango**

AKIWA ameiongoza kwenye mechi mbili tu, mabosi wa Simba wameonekana kufurahishwa na mwanzo mzuri wa Kaimu Kocha Mkuu wa timu hiyo, Juma Mgunda, wakisema ameleta hali ya upambanaji ndani ya kikosi chao, imeelezwa.

Simba itashuka dimbani kesho kuwakaribisha Nyasa Big Bullets, kutoka Malawi katika mechi ya marudiano ya Ligi ya Mabingwa Afrika itakayochezwa kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam.

Meneja Habari na Mawasiliano wa Simba, Ahmed Ally, alisema ujio wa kocha huyo umebadilisha hali za wachezaji ambayo haikuwepo kabla ya kocha huyo kuwasili ambapo sasa kila mmoja anapambana na kujituma tofauti na ilivyokuwa katika mechi tatu za mwanzo za Ligi Kuu Tanzania Bara.

Ahmed alisema, hata kwenye mechi dhidi ya Prisons, kama isingekuwa wachezaji kujituma na kupambana, bao lililopatikana dakika tano kabla ya mechi huenda lisingefungwa.

"Kwa kweli kocha Mgunda ameongeza ari kubwa ya kupambana, wachezaji sasa wanajituma mno, wanacheza 'jihad' kitu ambacho kilikosekana muda mrefu ndani ya Simba. Ukitazama mechi ya Prisons utaelewa kile ninachokisema. Katika mechi zetu tatu za mwanzo ulikuwa unaona, mbili tulishinda lakini hawakupambana, timu ilicheza kama bonanza hivi, walikuwa wanacheza kivivu, lakini angalia baada ya kuingia yeye, dhidi ya Nyasa Big Bullets walivyopambana, tazama dhidi ya Prisons. Siku ile dhidi ya Prisons kama siyo kupambana tusingepata bao, ufundi, mbinu zilikwisha.

Katika mechi hiyo hapo unahitaji mikimbio zaidi ya wachezaji, na ndiyo maana unaona hata goli limefungwa na Mkude (Jonas) ambaye ni kiungo mkabaji, na si mfungaji wa mara kwa mara, lakini kwa sababu ya kupambana na wenzake, wakafanikiwa," alisema Ahmed.

Ofisa huyo aliongeza Mgunda aliwakabidhi wachezaji jukumu la kupambana kwa ajili ya nembo ya klabu, wanachama na mashabiki, pamoja na kupambania yeye kocha.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >